UKURASA WA 2
**Taasisi** ya Profesa J yachangiwa mil. 15/-...



UKURASA WA 4
RIPOTI MAALUM
**Selimundu** janga jipya afya nchini...



UKURASA WA 5
**Majaliwa** aagiza madeni ya vyombo vya habari yalipwe...




**KLOPP AMSIFU NUNEZ KWA KIWANGO BORA**
UKURASA 22

# Nipashe


Jumanne Novemba 14, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581494



0745 700710 LIKE & FOLLOW US
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com


ATHARI YA MAFURIKO

# Timu ya mawaziri yatinga Jangwani



UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 5
**OFISA MIPANGO MIJI AKWEPA JELA MIAKA 2 KWA KULIPA FAINI**
MAHAKAMA ya Wilaya ya Ilala imemtia hatiani Ofisa Mipango miji, kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Melchiory Mukandala, kwa...

UKURASA WA 8
**LATRA YATAKA ABIRIA KUSAFIRI KWA VYOMBO VILIVYOKATIWA BIMA**
MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imewataka abiria kusafiri kwenye vyombo vya moto ikiwamo mabasi...

## Makonda aamuru gari lake la msafara kubeba mwili uliokwama kuzikwa

UKURASA 3



Magari yakiwa yamekwama katika barabara ya Msasani eneo la Morombo, jijini Arusha kutokana na kuharibika na mvua kubwa iliyonyesha jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Hatima wafanyakazi 279 wa KIA yawekwa wazi

UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA YAANIKA SIKU KOCHA MPYA KUTUA UK.24 **KATUNI** UK.6

# Timu ya mawaziri yatinga Jangwani

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa na Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, jana ilifika eneo la Jangwani kuangalia athari ya mvua na kuwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuwatembelea wananchi wote waliopata athari za mafuriko ili kuwapa msaada.

Mawaziri hao pia waliwaagiza mameneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) wa mikoa na wilaya nchi nzima kutembea kwenye barabara ili waone jinsi ya kuzirekebisha na kujenga zitakazodumu bila kuathiriwa na mafuriko.

Awali, wakazi wanaoishi kando ya Mto Msimbazi, jijini Dar es Salaam, ambao hawakufikiwa na fidia ya kuondoka maeneo yao wameiomba serikali kuwaangalia kwa kuwa wako tayari kuhama kutokana na athari za mafuriko.

Wananchi hao walisema mvua iliyonyesha juzi imeacha kilio kwa wanaoishi pembezoni mwa Bonde la Msimbazi, baada ya kubomoa nyumba na kuwaacha wakiwa hawana pa kwenda huku waliosalimika wakipata hasara kwa kuharibikiwa mali zao.

Serikali kwa upande wake imesema inajipanga upya ili kuhakikisha kuwa daraja jipya litakalojengwa eneo la Jangwani litadumu na kutosababisha mafuriko na usumbufu kwa wapitanjia kwa miaka 100.

Mkazi wa Mtaa wa Msimbazi Mama-Tabata, Wilaya ya Ilala, Baltaza Joseph, alimweleza mwandishi wa gazeti hili kuwa mvua iliyonyesha juzi imewaacha na umaskini mkubwa baada ya nyumba kubomoka na baadhi ya thamani zake kusombwa na maji.

Alisema tukio hilo lilitokea saa sita usiku na kuambulia kuokoa familia yake wakiwamo watoto na wakati wanataka kuokoa baadhi ya vitu vya thamani sebuleni na chumbani, ukuta wa vyumba ulianguka na maji kuingia ndani kwa nguvu na kuvisomba.

Tamasina Raymond, mkazi wa eneo hilo alisema nyumba anayoishi ilibomolewa na mvua iliyonyesha mwaka jana na kulazimika kujenga chumba kimoja ili ajihifadhi na mtoto wake kwa kuwa hana pa kwenda.

**KAULI YA MAWAZIRI**

Waziri wa TAMISEMI, Mchengerwa, aliwaelekeza wakuu wa mikoa na wilaya nchi nzima kuwatembelea wananchi, kukagua athari na kuwasaidia wahitaji.

Vilevile, aliwaelekeza mameneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) wa mikoa na wilaya nchi nzima kutembelea barabara na kuzirekebisha kwa kujenga za kudumu.

Alisema kwa kushirikiana na mkuu wa mkoa, wiki hii watawatembelea wananchi wa Msimbazi na kuzungumza nao ili waone namna gani watatekeleza hatua ya pili ya ujenzi wa matuta na mitaro kwa kuwa fedha tayari wanayo.

Waziri Mchengerwa alisema aliyejenga daraja la Jangwani ameiangusha serikali kwa kuwa imekuwa kinyume na matarajio ya kumaliza tatizo la maji kujaa na kusababisha mafuriko.

Alisema watatekeleza agizo la Rais Dk. Samia Suluhu Hassan lililoelekeza wizara yake, Wizara ya Ujenzi, Wizara ya Fedha na wataalamu kutoka Benki ya Dunia (WB), kukaa pamoja na kujadili namna ya kuboresha eneo la Jangwani ili mafuriko yasijirudie tena.

Waziri wa Ujenzi, Bashungwa, alimwagiza meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Dar es Salaam, kuhakikisha tope lote lililokuwa chini ya Daraja la Jangwani linazibuliwa ili maji yaweze kupita badala ya kujaa barabarani.

"Tumekuja hapa (Jangwani) tumeona changamoto ni taka kuziba chini ya daraja na wote mimi na Waziri Mchengerwa tunawaagiza ma-RC na ma-DC maeneo yote kusimamia na kutoa elimu kwa Watanzania kuzingatia usafi, ukiwa kwenye chombo chochote cha usafiri au unatembea kwa miguu, ukinywa maji sio ustaarabu kutupa chupa," alionya.

Novemba 21, mwaka jana, serikali ilisaini makubaliano na WB ya mkopo nafuu wa Sh. trilioni 1.24 kwa ajili ya ujenzi wa uendelezaji wa bonde la Mto Msimbazi utakaohusisha ujenzi wa daraja la kisasa la Jangwani pamoja na miradi ya umeme vijijini.

Aliyekuwa Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila, wakati huo alisema mwonekano wa daraja hilo utakuwa kama la Tanzanite na likikamilika litaandika historia mpya ya kusahau adha ya mafuriko maeneo ya Jangwani.

Jana Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alisema kwa sasa hali inaendelea vizuri kwa kuwa maji yaliyokuwa yanaleta usumbufu katika eneo la Jangwani yameisha na TANROADS wanaendelea na shughuli ya kutoa tope lililojaa chini ya daraja hilo huku akiwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari.



Miriam Abdallah (75) mkazi wa kitongoji cha Munyituka kilichopo kata ya Mtamaa Manispaa ya Singida akichota maji jana katika kisima ambacho ni miongoni mwa visima 38 vilivyokarabatiwa na Shirika lisilo la kiserikali la Empower Society Transform Lives (ESTL) kwa ufadhili wa Taasisi ya Mo Dewji Foundation. **PICHA; THOBIAS MWANAKATWE**

## Taasisi ya Profesa Jay yachangiwa milioni 15/-

**Na Elizabeth Zaya**

KATIKA kuchangia uzinduzi wa taasisi ya msanii wa Bongo fleva na mbunge wa zamani wa Mikumi (CHADEMA), Joseph Haule (maarufu Profesa Jay), Kiongozi wa chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe ameunga mkono kwa kumchangia Sh. milioni 10.

Profesa Jay alikuwa akisumbuliwa na maradhi ya figo na alitibiwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Wengine ambao wamechangia taasisi hiyo ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, walichangia Shilingi milioni tano kabla ya bunge hilo kuahirishwa mwishoni mwa wiki, siku ambayo msanii huyo alitembelea bungeni hapo.

Kwa mujibu wa Pofesa Jay, ameamua kuanzisha taasisi hiyo ili isaidie wagonjwa wa figo na anatarajia kuizindua rasmi mwezi huu (Novemba) Mliman City, jijini Dar es Salaam, lengo lake ni kukusanya Sh. milioni 800.

Akiwa kwenye kipindi cha televisheni cha Clouds, Zitto aliahidi kutoa mchango huo kwa kuuweka kwenye akaunti ya benki ya taasisi ya Profesa Jay.

"Mimi ndani ya siku mbili hizi nitakuletea Sh. milioni 10. Tayari nimechukua akaunti ya benki kwenye matangazo na naunga mkono juhudi yako, ni kazi kubwa ambayo unaifanya.

"Mwenyezi Mungu amekupa siku zaidi za uhai na amekuondoa kwenye mtihani mkubwa na wewe umeamua kulipa kwa kuwasaidia, kwa kweli ni lazima uungwe mkono," alisema Zitto wakati akizungumza na Profesa Jay kwenye simu.

"Na mimi kama mwenzako tumekuwa pamoja kwenye shughuli zetu za kisiasa na tumefanya kazi pamoja kama wabunge, lazima nikuunge mkono kwahiyo tegemea kunisoma, utasoma muamala huu ambao nimekuambia wa Sh. milioni 10."

Akizungumza hivi karibuni na televisheni hiyo, msanii huyo maarufu wa bongo flava, alisema akiwa kwenye matibabu yake hospitalini, alishuhudia wagonjwa wengi wa figo wakishindwa kumudu gharama za matibabu na kurudi nyumbani.

"Kwahiyo kwa namna tulivyoona watu wengi wakija hospitali na kushindwa kutoa sumu kwenye figo kutokana na ukubwa wa gharama za matibabu, tukaona tuanzishe taasisi kama hii inayolenga kusaidia katika eneo hilo," alisema Profesa Jay.

Kwa mujibu wa msanii huyo, alilala kitandani hospitali kwa siku 462 wakati madaktari wanapambania afya yake.

# Hatima wafanyakazi 279 KIA yawekwa wazi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

HATIMA ya wafanyakazi 279 wa Kampuni ya Usimamizi na Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO), imejulikana baada ya serikali kuwatangazia kuwa watakuwa chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA).

Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akizungumza jana na wafanyakazi hao, baada ya serikali kuurejesha rasmi chini ya usimamizi wa TAA, alisema wako salama zaidi kuliko huko nyuma.

"Hakuna mtu yeyote ambaye atapoteza kazi yake, atapoteza ajira yake, atapoteza stahiki zake hata mmoja. Wala watu wasiwe na wasiwasi kwamba wewe leo unapata mshahara mkubwa, na kwa sababu imeenda kule (TAA), utapata mshahara mdogo, hilo halipo...Naomba niwahakikishie nyote pamoja na familia zenu mko salama."

Kuvunjwa kwa KADCO na jukumu la uendeshaji na usimamizi kurejeshwa KIA, kunafanya idadi ya viwanja ya ndege nchini, vinavyoendeshwa na kuendelezwa na TAA kufikia 59.

Akifafanua kuhusu hatua inayofuata baada ya shughuli za KADCO kutwaliwa na TAA, Waziri Mbarawa, alisema:

"Hatua ya pili sasa ni jinsi gani tunataka kushughulikia mambo ya wafanyakazi kuyaweka vizuri. Utaratibu huko mbele tutaeleza ni utaratibu gani."

Kuhusu maboresho ya uwanja wa KIA, Waziri Mbarawa, alisema baada ya uamuzi wa serikali wa kuuondoa uwanja huo chini ya KADCO na kuwa chini ya usimamizi wa TAA, serikali sasa inaenda kufanya mabadiliko makubwa KIA.

"Mimi nikiangalia mbele miaka mitatu, ninaona kuna Terminal kubwa (uwanja) inakuja ya kisasa. Tangu miaka hiyo Terminal One ndiyo hii, hakuna mabadiliko. Uwanja wa ndege ambao duniani ukizingumza KIA, ukizingumza Ngorongoro ni hapa. Tumejaribu kuwapa (KADCO) miaka 25, lakini bado. Hatukusema hamkufanya vizuri, mmefanya vizuri, tena nawapongeza sana kwa kazi kubwa, lakini iko haja sisi twende mbele."

Mkurugenzi Mkuu wa TAA, Mussa Mbura, alisema wanaanza kazi mara moja kutokana na maelekezo ya waziri mwenye dhamana.




# Makonda aamuru gari lake la msafara kubeba mwili uliokwama kuzikwa

**Beatrice Shayo na Rose Jacob,**
MWANZA

MWILI wa marehemu Steven Busapali (39), mkazi wa Nyashishi, wilayani Misungwi mkoani Mwanza, uliodaiwa kuzuiwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Mwanza Sekouture kwa siku tano, kwa deni la Shilingi milioni mbili umekabidhiwa kwa ndugu zake.

Hatua hiyo imekuja baada ya ndugu wa marehemu kutoa malalamiko kwa Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, kuwa hawana uwezo wa kulipa fedha hizo ili wakabidhiwe mwili wa ndugu yao.

Makonda aliagiza ndugu hao kukabidhiwa mwili huo haraka na kutoa gari la wagonjwa lililokuwa kwenye msafara wake kwenda kuuchukua mwili huo na kupelekwa nyumbani kwake Nyashishi, wilayani Misungwi na kuzikwa Kijiji cha Nyahiti.

Akithibitisha kuchukuliwa kwa mwili huo, Mganga Mfawidhi wa hospitali hiyo, Bahati Msaki, alisema hakukua na mwili unaodaiwa Shilingi milioni mbili.

"Hakuna mtu yeyote aliyekuja kuchukua mwili akanyimwa, Novemba 12, alikuja ofisini ndugu wa marehemu akaomba gharama za matibabu za marehemu ambazo ni Sh. 1,065,000 tukampatia, akaondoka," alisema Msaki.

Alisema baada ya hapo ndugu huyo alisema atakuja kuuchukua mwili Novemba 13, hata hivyo, hawaelewi mtu huyo alikuwa na nia gani mpaka kuibukia kwa kiongozi," alifafanua Msaki.

Kaka wa ukoo wa marehemu, marehemu Steven aliyejitambulisha kwa jina la Thadeo Philipo, alisema wanaishukuru CCM, "maana tulipewa mwili wetu bure na usafiri hakuna gharama yoyote tuliyoitumia na leo (jana) Novemba 13 tulifanya mazishi ya ndugu yetu," alisema.

Akiwa kwenye mkutano wa hadhara katika viwanja vya ofisi ya CCM mkoani hapa, Makonda alisema, Serikali ya CCM itajenga barabara ya njia nne kutoka mzunguko wa jengo la CCM Mkoa wa Mwanza hadi mji wa Kisesa na Usagara, huku akiagiza kukamilika haraka jengo la abiria lililopo katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza.

"Hapa nilipo ninaona nyuso za wananchi nyingi zimejaa shauku ya kutoa kero, sasa ninaziagiza kamati za siasa za mikoa na wilaya kuzisimamia halmashauri.

"Kutokana na watumishi kushindwa kufuata maadili, ndiyo maana rushwa zinashamiri, hivyo watakaobainika wachukuliwe hatua hususani katika sekta ya ardhi," alisema Makonda.

Akiwa wilayani Magu, Makonda alisema CCM kitaendelea kuimulika serikali na kuelekeza kuchukuliwa hatua watumishi wazembe, wala rushwa na wasio waaminifu wa mali za umma ili fedha ya mwananchi anayelipa kodi na anazotoa Rais Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya maendeleo ziwe na tija kwa wananchi.

Akizungumza na wananchi wa eneo la Kisesa, wilayani Magu, mkoani humo alisema

chama hakitoi dhamana ya kuongoza kwa kuangalia watu, wadhifa wala dini ya mtu bali kinaangalia uwezo wa mtu katika kutatua kero za wananchi na kuleta maendeleo.

Makonda alisema katika kuhakikisha kero mbalimbali zinatatuliwa, serikali inatekeleza miradi mingi ya maendeleo ikisimamiwa na viongozi hao licha ya kukiri kuwapo baadhi ya wazembe ambao wanakwamisha juhudi hizo.

"Wapo watu wazembe, wala rushwa ni jukumu letu kama chama kuendelea kuimulika serikali na kuisimamia kikamilifu ili fedha ya mwananchi anayelipa kodi na fedha za kiongozi wetu anazozitoa kwa ajili ya maendeleo iwaletee tija wananchi," alisema Makonda.

Alisema kiapo cha chama na msingi wake ni binadamu wote sawa, hivyo wanataka uadilifu uliotukuka ikiwamo utoaji wa huduma stahiki kwa wananchi.

"Tunataka uadilifu uliotukuka, ukienda hospitali uhudumiwe kikamilifu, ukienda manispaa au halmashauri uhudumiwe kikamilifu, usihudumiwe kwasababu umesoma au una pesa, au una ndugu kiongozi, bali uhudumiwe kwasababu wewe ni binadamu na kiapo chetu kina sema binadamu wote ni sawa na huo ndio msingi wa CCM," alisema Makonda.

"Hizi shule ambazo Rais wetu ameleta fedha kwa sababu ya ongezeko la watu shule moja haitoshi na madawati hayatoshi, serikali yetu imekubali kubadilika kulingana na mahitaji ya wakati tukaletewa fedha tukajenga madarasa na watoto wetu wanaenda shule," alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA FEDHA**
**CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI**

Toleo Na. 70

2023

# TAARIFA KWA UMMA

## MAHAFALI YA 37 YA CHUO

*Tarehe; 14/11/2023*

Chuo Cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kinawataarifu wahitimu wote wa Mwaka wa Masomo **2022/23** na Umma kwa ujumla kuwa sherehe za Mahafali ya 37 ya Chuo zitafanyika siku ya Ijumaa tarehe **24/11/2023** kuanzia saa 3:00 asubuhi katika ukumbi wa Mwl. J.K. Nyerere kwa Kampasi Kuu Dodoma, na siku ya Ijumaa tarehe **8/12/2023** kwa Kituo cha Mafunzo ya Kanda ya Ziwa - Mwanza.

Wahitimu wote watakao shiriki kwenye Mahafali haya wanapaswa kuzingatia yafuatayo: -

1. Mhitimu anayetaka kushiriki mahafali haya athibitishe ushiriki wake kupitia kiunganishi hiki **https://grs.irdp.ac.tz** . Majoho yatatolewa Chuoni Kampasi Kuu Dodoma kuanzia tarehe **20/11/2023** hadi tarehe **23/11/2023** na Kituo Kanda ya Ziwa Mwanza majoho yatatolewa kuanzia tarehe **04/12/2023** hadi **07/12/2023;**

2. Gharama ya kuazima joho ni Sh. **40,000/=.** Fedha hii italipwa kupitia "Control Number" itakayo tolewa kwa kila mhitimu. Mhitimu akirejesha joho atarudishiwa Sh.**10,000/=.** Endapo mhitimu atashindwa kurejesha joho ndani ya siku mbili atalazimika kulipa Sh **10,000/=** kila siku;

3. Kwa Kampasi Kuu **"rehearsal"** itafanyika siku ya Alhamisi tarehe 23/11/2023 kuanzia saa 9:00 alasiri katika ukumbi wa Mwl. J.K.Nyerere baada ya kuisha kwa ***"Convocation"***. Kwa Kituo cha Mafunzo cha Kanda ya Ziwa- Mwanza **"rehearsal"** itafanyika Siku ya Alhamisi tarehe 7/11/2023 katika Viwanja vya Chuo, Kitumba - Kisesa, Mwanza;

4. Mahafali haya yatatanguliwa na Kongamano la 16 la Kitaaluma (the 16th Convocation) litakalofanyika **Miyuji North maarufu 40 Acres (LT8)**, Kampasi Kuu - Dodoma siku ya Alhamisi tarehe **23/11/2023** kuanzia saa 3.00 asubuhi. Moja ya shughuli za tukio hili itakuwa utoaji wa tuzo kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika nyanja za masomo, michezo,ubunifu, na uongozi. Kwa Kituo cha Mafunzo cha Kanda ya Ziwa - Mwanza wanafunzi waliofanya vizuri katika nyanja za masomo, michezo, ubunifu, na uongozi watatunukiwa tuzo zao wakati wa mahafali yatayofanyika tarehe 8/12/2023. Orodha ya wanafunzi hawa inapatikana kwenye tovuti ya Chuo **www.irdp.ac.tz .**

**"KUPANGA NI KUCHAGUA"**
**Imetolewa na,**

**Godrick H.B.Ngolly**
**MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO NA MASOKO**

177112

**RIPOTI MAALUM**

# Selimundu; janga jipya afya nchini

## •Kila siku watoto 39 wanazaliwa wakiwa na ugonjwa huo
## •Kanda ya Ziwa yaongoza, madaktari bingwa watoa hadhari
## •Kutibiwa milioni 40/-, aliyepoteza wanawe wawili alonga

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

KILA siku watoto 39 wanazaliwa wakiwa na ugonjwa wa selimundu nchini. Kati yao, 28 (asilimia 72) huzaliwa mikoa ya Kanda ya Ziwa huku Mkoa wa Mwanza pekee ukiwa na wastani wa watoto watano kwa siku.

Aman Stanslaus (36), mkazi wa Nyamagana, mkoani Mwanza, anakumbuka yaliyomsibu miaka tisa iliyopita huko Busega mkoani Simiyu alipopoteza wanawe wawili kutokana na ugonjwa huo mwaka 2018 huku mumewe akitengana naye.

Mama huyo ambaye kitaaluma ni mwalimu, anasimulia kuwa baada ya miaka minne ya ndoa yake na mwalimu mwenzake (jina tunalihifadhi), walifanikiwa kupata mtoto anayemtaja aliongeza furaha kwao, pia kwa ndugu na marafiki.

Hata hivyo, furaha hiyo ilidumu kwa miaka minne. Mwaka 2018, mtoto wao, akiwa shuleni aliripotiwa na walimu kwamba alikuwa na maumivu kwenye maungo ya mwili, wakalazimika kwenda kumchukua katika shule hiyo ya bweni, wakampeleka hospitalini.

Akizungumza kwa sauti ya chini na kuna hatua anasita kuendelea na mazungumzo na kuhamia kwenye kilio, Mwalimu Aman anasimulia kilichojiri hospitalini na nyumbani, akitamka:

"Baada ya vipimo katika Hospitali ya Wilaya ya Magu, madaktari walituambia kuwa mwanangu anasumbuliwa na homa, lakini baada ya muda akawa ameishiwa damu, wakamwongeza.

"Tukaruhusiwa kurejea nyumbani, lakini baadaye akaishiwa damu tena ndipo madaktari wa hospitali hiyo walipojiuliza 'kwanini anaishiwa damu kwa muda mfupi baada ya kuongezwa?'. Wakalazimika kumpima sikoseli (selimundu) na majibu yalipotoka alibainika kuwa 'positive' (chanya, yaani alikuwa na ugonjwa huo).

"Sikuwa na uelewa wa ugonjwa huu, lakini mtoto alianza kupatiwa matibabu na alirejea shuleni. Ghafla hali ilibadilika na kuishiwa damu. Hapo ndipo shida zilipoanzia; kutokuelewana ndani ya familia, kila mtu akimwuliza mwenzake hili tatizo lipo upande wa nani, pasipokutarajia tuhuma zote zilielekezwa kwangu.

"Hapo ndipo matibabu yakahamia kwenye miti shamba, lakini mimi sikuwa na mrengo huo. Mume wangu na familia yake walijikita katika imani hiyo. Mimi nikajikita katika huduma za hospitalini japokuwa kuna wakati walilazimika mpaka kumleta mganga wa kienyeji nyumbani kwa ajili ya kutoa huduma kwa mtoto."

Mwalimu huyo anabainisha kuwa wakati wakiendelea na matibabu ya mtoto wao huyo, alijifungua mtoto mwingine. Naye akawa na selimundu. Wakamwanzishia kliniki ya matibabu ya ugonjwa huo katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando.

"Baadaye nikapata mimba nyingine ya mtoto wa tatu. Wa kwanza aliendelea kusumbua na vurugu ziliongezeka nyumbani, maelewano yakatoweka. Mume wangu aliungana na familia yake na kusema mimi ni chanzo na hawakuamini kwamba ni sikoseli. Walidai ni 'chango' (ugonjwa unaowapata watoto unaofanana na degedege).

"Mtoto wa pili naye alizidi kuumwa, nikashauriwa na madaktari wa Hospitali ya Wilaya ya Magu nimpeleke Bugando pia akaangaliwe. Mume wangu na ndugu zake waliitakaa rufani ya kwenda Bugando, mimi nikaipokea.



Jinsi selimundu ilivyo

"Tuhuma nyingi zilielekezwa kwangu; mara nilipenda kwenda kutembea mjini pasipo kuangalia hali ya mtoto wa kwanza ambaye alipooza kwa siku 14 akiwa haongei, wao walitaka atibiwe kwa dawa za kienyeji.

"Baadaye mtoto akapatwa na degedege. Nilikwenda naye Bugando, nilikaa naye kwa muda wa siku saba, wakamfanyia vipimo ikaonekana figo imeharibika sana kutokana na matumizi holela ya zile dawa za kienyeji. Ikawa ndiyo safari yake ya mwisho duniani... alipoteza maisha.

"Wakati huyo mwanangu akiwa mahututi hospitalini, yule wa pili aliomba kwenda hospitalini kumwona ndugu yake, kipindi hicho naye alikuwa anatibiwa nyumbani kwa miti shamba, wakamkatalia, alilia hadi akapoteza fahamu. Akalazwa katika kituo cha afya kilichoko maeneo hayo, lakini alipozidiwa tukalazimika naye kumpeleka Bugando.

"Hapo nikawa na watu wawili; mmoja mochwari mwingine chumba mahututi kwa wakati mmoja. Nilikwenda kuzika na baadaye nikarudi kumwuguza huyu mwingine. Hapo familia hatuelewani kabisa.

"Niliamua kuomba uhamisho ili niwe karibu na hospitali hii kwa ajili ya matibabu ya mtoto ambaye alikata kauli tangu kipindi kile akihitaji kumwona ndugu yake, ilimchukua miezi mitatu akiwa anakula kwa mpira. Miezi mitatu baada ya mwenzake kufariki (dunia) naye akaaga dunia... (simanzi inamtawala, analia)."

Baada ya takriban dakika tano, mama huyo anaendelea na mazungumzo na mwandishi, akisimulia: "Baadaye nikajifungua mtoto wa nne. Daktari (wa Bugando) alinishauri niwapime watoto waliobaki hai. Majibu yalipotoka, mtoto wa tatu alionekana kuwa na sikoseli na wa mwisho alikuwa mzima kabisa.

"Daktari alishauri waanze kumshughulikia huyu mtoto wa tatu. Kipindi hicho nilikuwa ninalea mwenyewe. Tulitengana na baba yao kutokana na kunituhumu kwamba mimi ni chanzo kwa vyote vilivyotokea. Alitoa kauli kali kwamba 'heri watoto hao wamefariki dunia maana wamemgharimu kiuchumi," anadai Mwalimu Aman.

Mama huyo anasema anazingatia kliniki ya mwanawe huyo. Tangu aanze matibabu hayo miaka minne iliyopita, hajawahi kuongezwa damu na amelazwa mara mbili. Watoto wanapougua hatoi taarifa kwa mzazi mwenziwe ingawa alitumia njia za kisheria kupata matumizi ya watoto hao toka kwa baba yao.

Vilevile, Mwalimu Aman anabainisha kuwa hakuwahi kufanya uchunguzi wa afya yake. Baada ya kupata matatizo hayo, alipima na majibu yalibainisha ana hali anayoiita AS, ikiwa na tafsri ya kitabibu kwamba ni mtu mwenye vinasaba vya sikoseli.




Mwalimu Aman Stanslaus na mwanawe anayeugua selimundu, Anhonia Bundala

Kukabiliana na baa la selimundu Kanda ya Ziwa na Tanzania kwa ujumla, mama huyo anashauri watu wanaoingia katika uhusiano wapime kwanza hali ya vinasaba vyao na kutokupendana kwa macho tu kwa kuwa athari itakayomkuta mtoto watakayemzaa ni kubwa na wakikaidi wakubaliane na matatizo watakayokutana nayo.

"Nilipitia wakati mgumu mno baada ya kutengana na mume wangu. Kama si ndugu zangu kunishika mkono, sidhani kama leo tungekuwa tunaongea hapa, bila shaka nisingekuwa hai.

"Sikuwa na makazi baada ya kutengana na mume. Nyumba tuliyokuwa tunaishi nilishiriki kwenye ujenzi wake, nilichukua mkopo benki. Tulipotengana nililazimika kuhama eneo hilo na mahala pa kazi ili kuwa karibu na hospitali. Mume wangu alishaoa na ana maisha yake mengine kwa sasa.

"Baada ya kuchukua mkopo huo, matatizo yalinikuta sipo vizuri kiuchumi, mpaka sasa bado hali yangu si nzuri kabisa. Hii nyumba ninamoishi nimefadhiliwa, ni kwa mjomba wangu. Bila ndugu zangu sijui ningekuwa wapi, wao ndio wananipa mpaka nguo, yaani acha tu!

"Maisha ni kumshukuru Mungu, ninaendelea vizuri japokuwa ikitokea mtoto akaumwa, nikapewa wodi, huwa ninashtuka sana kwa sababu ninawakumbua wale watoto wangu wawili wakiume niliowapoteza," anasema Mwalimu Aman na kutoa rai kwa jamii iondokane na dhana kuwa watu wenye selimundu hawawezi kuishi na kuwachukulia ni watu wa kufariki dunia wakati wowote.

Pia, anaiomba serikali itoe elimu kwa jamii ili iwe na uelewa kuhusu ugonjwa huo kama magojwa mengine sambamba na kupunguza gharama za matibabu hasa upandikizaji uroto pamoja na kuwa na wataalamu wa wagonjwa huo hadi ngazi ya vituo vya afya na zanahati.

"Matibabu ya kuponesha sikoseli yanapatikana lakini ni gharama kubwa, waathirika wengi hawawezi kumudu. Mimi pamoja na kwamba ni utumishi wa umma na nina bima ya afya, haikuwa rahisi kumudu matibabu ya wanangu.

"Serikali iingie kati kupunguza gharama hizo, pia bima nayo iweze kuchangia kiasi kwenye matibabu hayo kwani kupata zaidi ya Sh. milioni 60 hadi 65 ambazo ni gharama za awali ni tatizo," Mwalimu Aman anahitimisha.

Mwandishi wa habari hizi alizungumza na mtoto wa mama huyo anayeugua selimundu, Anthonia Bundala (9), msichana anayesoma darasa la IV katika Shule ya Msingi Nundu iliyopo wilayani Ilemela mkoani Mwanza. Walimu wake wanamtaja ana maendeleo mazuri darasani. Mwenyewe ana ndoto ya kuwa daktari ili kuwasaidia watu wengine wenye ugonjwa huo.

"Ninamshukuru sana Mungu, mamaangu, ndugu zangu na marafiki zangu shuleni, wananipenda sana. Ninapenda kusoma na mama ananisaida, nina imani ndoto yangu nitaifikia ya kuwasaidia watu wengine wenye ugonjwa kama wangu nitakapokuwa daktari, anasema mwanafunzi huyo.

**Itaendelea Kesho**

## Ofisa mipango miji akwepa jela miaka 2 kwa kulipa faini

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Ilala imemtia hatiani Ofisa Mipango miji, kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Melchiory Mukandala, kwa makosa mawili ikiwamo kutumia madaraka yake vibaya.

Hukumu hiyo ilitolewa jana mbele ya Hakimu Mkazi, Fahamu Kibona, baada ya kupitia ushahidi wa pande zote mbili na kujiridhisha kwamba upande wa Jamhuri umethibitisha mashtaka bila kuacha shaka.

Mukandala alihukumiwa kwenda jela miaka miwili au kulipa faini ya Shilingi milioni mbili, baada ya kutiwa hatiani kwa makosa mawili, likiwamo kutumia madaraka yake vibaya kwa kuvunja Sheria ya Ardhi.

Mshtakiwa alitiwa hatiani kwa kosa la kughushi barua za marekebisho ya umiliki na kusababisha Audax Mhali na mkewe Magdalena Mhali kuongezewa eneo mara mbili katika kiwanja kilichokuwa mtaa wa Mogo, Kata ya Kipawa, Dar es Salaam, kinachomilikiwa na watoto wa marehemu Ally Kwaro.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kibona, alisema upande wa Jamhuri wakati wa usikilizwaji wa shauri hilo walikuwa na mashahidi wanane na vielelezo vinane na kuthibitisha mashtaka yote mawili bila kuacha shaka yoyote.

Akisoma sehemu ya ushahidi uliotolewa ukiwamo wa Mwenyekiti wa Serikali za Mtaa wa Mogo, Kata ya Kipawa, Dar es Salaam, ulieleza kuwa wakati wa uongozi wake hajawahi kushirikishwa wala kuona watu kutoka Wizara ya Ardhi kuhusu mabadiliko ya kiwanja hicho.

Ushahidi uliotolewa na mtumishi kutoka Wizara ya Ardhi, ulidai kwamba hawakuwa na barua ya kumbukumbu katika jalada lao kuhusu mabadiliko ya ardhi yaliyofanyika wala barua ya mwombaji akiomba kuongezewa eneo la mraba kutoka 244 hadi 695.

"Ushahidi uko wazi, unathibitisha mshtakiwa hakufuata taratibu zinazotakiwa kwani hata Wizara ya Ardhi wenyewe baada ya kupokea malalamiko kutoka katika familia ya marehemu Ally Kwaro, waliandika barua kwenda Manispaa ya Ilala Ili kupata ufafanuzi zaidi.

"Hatua hiyo imeonyesha taratibu za kubadilisha ardhi hazikufuatwa kwani barua ilikuwa siyo ya kiofisi bali mshtakiwa alijiandikia mwenyewe, alitakiwa kufuata mchakato ili aweze kuandika barua hiyo ya kuruhusu Manispaa ya Ilala kufanya mabadiliko hayo," alisema Hakimu Kibona.

Alisema Mahakama ilitegemea upande wa utetezi ungeleta mashahidi ambao ni Audax Mhali na mkewe Magdalena Mhali kama walipeleka barua wizarani Ili yafanyike marekebisho ya umiliki, lakini hawakufanya hivyo.

Hakimu Kibona, alisema baada ya ushahidi huo mahakama inaona mshtakiwa ana hatia kwa makosa yote mawili kama alivyoshtakiwa. "Shtaka la kwanza mshtakiwa anatakiwa kulipa faini Shilingi milioni moja au kwenda jela miaka miwili na shtaka la pili kulipa faini Shilingi milioni moja au jela miaka miwili," alisema.

Hakimu Kibona, alisema adhabu ya kwenda jela inakwenda kwa pamoja ambayo ni miaka miwili jela, hata hivyo mshtakiwa alifanikiwa kulipa faini ya Shilingi milioni mbili na kuepuka adhabu ya kwenda jela miaka miwili.

Kabla ya kutolewa kwa adhabu hiyo, mawakili kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Hassan Dunia na Gloria Mwainyekule, waliomba mahakama itoe adhabu kali kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwa watumishi wengine wa serikali kwa kuwa vitendo hivyo vinaleta dhamira mbaya kwa jamii akiwa ni mfanyakazi wa serikali.

Wakili wa utetezi, Kelvin Rubago, aliomba mahakama impunguzie adhabu mteja wake kwa kuwa ni mkosaji wa mara ya kwanza na ana matatizo ya kiafya kutokana na kupata kiharusi.

# Jafo aridhishwa utunzaji wa mazingira kiwanda Pwani

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amewataka wamiliki wa viwanda nchini kuzingatia kanuni kwa kuwaepusha wananchi na uchafuzi wa mazingira wa moshi wa viwandani.

Alitoa agizo hilo jana mkoani Pwani, wilayani Mkuranga alipotembelea kiwanda cha Lodhia kinachojihusisha na uzalishaji wa nondo na bidhaa za plastiki kuona kama walitii maagizo ya kuzingatia kaununi ya usafi wa mazingira aliyoyatoa awali.

Aliutaka uongozi wa kiwanda hicho kuzuia moshi na kujenga sehemu maalum ya kuhifadhi vyuma chakavu.

Akiwa ameambatana na Kamati ya Kudumu ya Bunge, Maji na Mazingira, alisema kiwanda hicho kimetekeleza maagizo yake kwa asilimia 100.

"Nilikuja nilitoa maagizo wahakikishe moshi hautiririki, watengeneze eneo maalum la kuhifadhia vyuma chakavu na ninawashukuru sana wamefuata maagizo kila kitu kipo sawa na hali ni nzuri.

"Moshi ukitiririka ukienda angani unasababisha ongezeko la joto, niwatake wamiliki wengine wa viwanda waige mfano huu kwa kutunza mazingira."

Mkurugenzi wa Lodhia, Sailesh Pandit, aliishukuru serikali kwa kutembelea kiwanda chake na kuahidi kuendelea kufuata miongozo waliyopewa.

Aliitaja changamoto inayowakabili katika uzalishaji wao kuwa ni pamoja na uhaba wa vyuma chakavu.

"Kuhusu changamoto hiyo nimemuomba waziri tuangalie sana hili suala la vyuma chakavu kuuzwa nje ya nchi kwa sababu ndio vinatumika kutengeneza hizi bidhaa.

"Serikali iangalie namna ya kusitisha utoaji wa vibali hivyo, lakini pia iangalie namna gani huko mipakani watazuia visiende kuuzwa nje," alisema.

Alisema kiwanda hicho kwa sasa kimeajiri Watanzania 1,069 kati yake wanawake 167 na mpango walionao kwa sasa ni kuajiri zaidi madereva wakike kutoka vyuo vya Veta.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Maji na Mazingira, Anna Lupembe, Mbunge wa Nsimbo Katavi, alisema ameridhishwa na kiwanda hicho kilivyotii agizo la serikali.

"Haya ni mafanikio makubwa sana katika nchi yetu, maagizo yote aliyoagiza Waziri Jafo yote yametekelezwa zamani kiwanda hiki kilikuwa kinatoa moshi, lakini kwa sasa hakuna hali hiyo," alisema.

Mbunge wa Jimbo la Makambako, mjumbe wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Deo Sanga, alikishauri kiwanda hicho kuiomba serikali ili iwapatie kitalu katia eneo la Liganga na Mchuchuma, Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe waweze kuchimba vyuma vitakavyo wasaidia katika uzalishaji wao.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (wa pili kushoto), akimsikiliza Faraja Ng'ingo Meneja wa NMB Kanda ya Kusini kabla ya kuzindua Mkutano Mkuu wa Saba wa Jukwaa la Wahariri (TEF) unaofanyika Lindi. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zainab Telack. **PCHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Majaliwa aagiza madeni ya vyombo vya habari yalipwe

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ifanye uratibu wa madai ya vyombo vya habari, sambamba na kuweka mfumo endelevu wa kutatua changamoto hiyo pamoja na nyinginezo zinazoikabili tasnia hiyo.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Saba wa Mwaka wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) katika Uwanja wa Ilulu, mkoani Lindi na kuwasisitiza wanahabari wafanye kazi kwa kufuata sheria za nchi kwa kutambua mazingira ya kazi na kuweka tahadhari zote.

Alisema taasisi za serikali zinaposhindwa kulipa madeni yanayodaiwa na vyombo vya habari, zinasababisha hasara na kudhoofisha uchumi wake, hali inayochangia kuyumba.

"Taasisi zote za serikali ziandae mpango wa kuhakikisha kuwa madai yote halali yanawekewa utaratibu maalum wa kuyalipa kwa sababu kuacha kulipa madeni haya ni kudhoofisha uchumi wa vyombo vya habari."

Pia, aliwataka wanahabari wahakikishe wananchi wanapata habari zilizo sahihi na zinazohamasisha maendeleo ili kuwe na kuchochea kufanya kazi kwa bidii.

"Tunawahitaji sana hususan katika kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo nchini, wananchi msiwabughudhi wala kuwashambulia wanahabari wakiwa wanatekeleza majukumu yao. Kuwashambulia waandishi wa habari ni uhalifu kama uhalifu mwingine.

Alisema serikali inatambua na kuthamini mchango wa vyombo vya habari katika kuitangaza nchi kitaifa na kimataifa pamoja na kuitangaza miradi inayotekelezwa na serikali kwa wananchi.

"Mheshimiwa Rais amenituma niwahakikishie kuwa wakati wote anapotekeleza majukumu yake, anatambua na kuthamini mchango wa vyombo vya habari nchini na anategemea sekta hiyo kuwa na mchango mzuri katika utekelezaji wa majukumu ya serikali nchini," alisema.

Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Mathew Kundo, alisema wizara hiyo inaendelea kuimarisha ushirikiano mzuri uliopo baina ya serikali na vyombo vya habari nchini.

"Katika kuhakikisha kunakuwa na uhusiano mzuri baina ya serikali na vyombo vya habari Mheshimiwa Rais, alielekeza kufanyika kwa mapitio kwa sheria zote zilizokuwa na upungufu na kulalamikiwa na wadau ikiwamo Sheria ya Habari ya Mwaka 2016," alisema.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, aliishukuru serikali kwa namna inavyoshughulikia changamoto mbalimbali katika sekta ya habari ambazo zimekuwa zikiwasilishwa muda mrefu na kuweka mazingira rafiki ya utendaji kazi kwa sekta ya habari.

"Leo hatuna malalamiko, ila tuna shukurani kwa namna ambavyo serikali imefanyia kazi malalamiko na changamoto zetu, sheria kandamizi ambazo tumekuwa tukizipigia kelele muda wote sasa serikali imezifanyia kazi," alisema Balile.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi epukeni kukimbilia hatari

**NI** jambo la kawaida hapa nchini baadhi ya watu wanapoona jambo la hatari kulikimbilia badala ya kuliepuka.

Yanapotokea matukio tofauti ya majanga yawe ya ajali, moto na mafuriko baadhi ya wananchi hao hutoka kwenye maeneo yao na kukimbilia kwenye hatari.

Hali hii imeshuhudiwa mara nyingi na husababisha madhara makubwa kutokana na hao wanaokimbilia majanga hayo kukumbwa na madhara.

Kama ilivyotokea ajali ya kuwaka moto gari la mafuta eneo la Msamvu, mkoani Morogoro miaka iliyopita, watu wengi walipata madhara ya kupata ulemavu wa maisha na wengine kupoteza maisha kwa sababu ya kukimbilia hatari kwa kutaka kupata bidhaa iliyomwagika kutoka kwenye ajali hiyo.

Wengine hukimbilia kwa nia njema ya kwenda kuokoa watu waliopata ajali, lakini wengine huenda kwa nia ya kupora mali zilizomo kwenye magari hayo.

Sababu ya kutoa tahadhari, ni tukio la mvua kubwa iliyonyesha Jumapili na kusababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu na mali za watu.

Hata hivyo, ni jambo la kumshukuru Mungu kwasababu hakuna kifo kilichoripotiwa baada ya kushuhudia maeneo mengi ya Jiji la Dar es Salaam yakiwa yamejaa maji hadi kufunika baadhi ya nyumba.

Jambo la kushangaza ni kitendo cha baadhi ya wananchi kutoka kwenye nyumba zao kwa usalama wao na kukimbilia kwenye maeneo yaliyofurika maji yanayoenda kwa kasi.

Tena wengine wakishangilia kama wameona kitu cha kufurahisha na baadhi wakidiriki kuokota chupa tupu za maji ambazo zilikuwa zimesombwa na mafuriko hayo.

Kila mara wananchi wanaelimishwa kuhusu kujiepusha kukimbilia majanga kwasababu wanaweza kuingia kwenye madhara makubwa.

Maeneo yaliyokumbwa na mafuriko kwa mfano Barabara ya Bagamoyo kuanzisha Boko Basihaya hadi kwenye daraja la Nyakasangwe, nyumba nyingi na sehemu za biashara ziliathirika na mafuriko ya mvua hiyo kubwa na wengine kubaki bila makazi.

Hata hivyo, baadhi ya wananchi walionekana kutoka kwenye nyumba zao ambazo ziko salama na kukimbilia barabarani ambako kulikuwa kumefunikwa na maji na wengine kufanya mchezo wa kukatisha kwenye maji hayo bila kujali kuwa yanaweza yakawasomba.

Maji ya mafuriko sio ya kuyafanyia mchezo yana nguvu kubwa ndio maana maeneo mengine yamebomoa nyumba kwasababu ya kutaka njia ya kupita.

Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), kila mara inatoa tahadhari inapokuwa inatoa utabiri wa hali ya hewa kwa kuwataka wananchi kuwa makini na wale wanaoishi mabondeni kutakiwa kuhama ili kunusuru maisha hayo.


Hata hivyo, baadhi ya watu huonekana kupuuza ushauri huo na kuendelea kuishi kwenye maeneo hayo mpaka wanapopata majanga huanza kuomba serikali iwasaidie kuwaokoa na kuwapelekea misaada.

Miaka ya nyuma wakati mvua ya El-Nino iliponyesha na kuleta madhara makubwa, watu waliokuwa wakiishi Jangwani walipewa msaada wa viwanja na serikali eneo la Mabwepande, pamoja na mifuko ya saruji na mabati, lakini wengi wao waliuza viwanja hivyo na kurudi kuishi mabondeni.

Linapotokea janga, watu hao hao huanza kuilaumu serikali kuwa haiwajali watu wake kwa kuwaacha wakiteseka kwenye mafuriko.

Watanzania lazima tujifunzie kusikiliza ushauri unaotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa na kuufuata. Wenzetu kwenye mataifa yaliyoendelea, hawawezi kutoka kwenye nyumba zao bila kwanza kusikiliza utabiri wa hali ya hewa ili waweze kujiandaa na vifaa vya kuwakinga.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Iwe mitihani isiyo na udanganyifu

**WATAHINIWA** 572,338 walianza kufanya mtihani wa taifa kidato cha nne jana kwa Tanzania Bara na visiwani. Tunawatakia kila la heri ili taifa liwe na wahitimu ambao kwa uaminifu wataitumikia nchi yao katika sekta mbalimbali.

Wakati huu wanafunzi hawa wakiandaliwa ili kuvushwa kuelekea hatua nyingine ya juu kwenye daraja la taaluma macho na masikio ya watu yanaelekezwa kwenye usalama wa mtihani kwa sababu yamejengeka mazoea ya baadhi ya wanafunzi, walezi, wazazi na walimu ambao siyo waaminifu kutumia mbinu mbalimbali kuiba mitihani kuanzia ya darasa la saba hadi taasisi za elimu ya juu.

Wakati watoto hawa wanapoingia kwenye vyumba vya mitihani yanatolewa onyo kwa wale ambao watajihusisha na udanganyifu, kwamba hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), Dk. Said Mohamed, anawataka wadau wa elimu wakiwamo wazazi, kwamba watakapoona vitendo vya udanganyifu vikifanyika, wapige simu namba 0759360000 au watume ujumbe kwa barua pepe "mailto:esnecta@necta.go.tz" esnecta@necta.go.tz kwa hatua zaidi.

Wakati Baraza la Mitihani likitangaza hatua hizo, ninadhani ipo haja kwa wanafunzi wenyewe kujiongeza na kuachana na mtindo wa udanganyifu, badala yake watumie maarifa waliofundishwa.

Baraza linatoa onyo kwa sababu imekuwa ni kawaida ya kuwapo kwa udanganyifu wa mitihani kila mwaka, jambo ambalo kwa namna moja au ngingine linachangia kuporomosha elimu.

Kwa mfano, kwenye mtihani wa kidato cha mwaka jana, shule nne zilibainika kufanya udanganyifu katika mikoa ya Dar es Salaam Mwanza, Mara pamoja na Zanzibar.

**Kwa mfano, kwenye mtihani wa kidato cha mwaka jana, shule nne zilibainika kufanya udanganyifu katika mikoa ya Dar es Salaam Mwanza, Mara pamoja na Zanzibar.**

Pamoja na hayo, ninadhani ipo haja pia ya wazazi na walezi kuwalea watoto katika maadili mema, ili watambue kuwa udanganyifu si mzuri na una madhara makubwa katika upande wa haki, maadili na uweledi.

Ninaamini wazazi na walezi wanapowapeleka watoto wao shule, wanataka wajifunze waelewe, ili baadaye watumikie taifa, lakini sio sahihi mtu anakuwa daktari, mhandisi au rubani kwa kuiba mtihani.

Jamii imekuwa ikishuhudia kuwapo kwa vitendo vya udanganyifu katika mtihani kwenye shule za msingi au sekondari, huku sababu zikielezwa kuwa ni wahusika kupata maslahi binafsi kupitia kile kinachoweza kuitwa kuwa ni biashara ya ufaulu.

Yaani kuanzia mzazi, mwalimu, mmiliki wa shule, msimamizi wa mitihani, mwanafunzi mwenyewe na hata baadhi ya maafisa wa vyombo vuya dola, kwa namna tofauti tofauti hudaiwa kuhusika katika mchezo huo mchafu wa ufaulu pasipo elimu.

Kimsingi mzazi anatamani mtoto wake afaulu vizuri, ili aweze kupata nafasi ya kujiunga na shule bora za sekondari za serikali, hasa zile zinazoitwa shule maalum za vipaji na ujiunga na vyuo vikuu.

Mwalimu naye anatamani wanafunzi wake wapate ufaulu wa juu ili kujenga jina lake na kutengeneza soko la ajira yake na mshahara mnono, ambao utakuwa unapanda kulingana na tija yake ya ufaulu wa wanafunzi katika somo analofundisha.

Haya ni baadhi ya maeneo ambayo yanaweza kuwa chanzo cha kuwapo kwa vitendo vya udanyanyifu na wizi wa mitihani kila mwaka unapoofanyika mitihani ya kuhitimu.

Ninatambua juhudi zinazofanywa na serikali na hatua mbalimbali ambazo inachukua kwa ajili ya kukabiliana na tatizo hilo la kufanya udanganyifu wa mitihani, lakini ni muhimu kuziba mianya niliyoitaja.

Matamanio ya wazazi, walezi na walimu na kutaka wanafunzi wafaulu, ni mazuri, lakini yasiwe chanzo cha kufanya udanganyifu, badala yake juhudi za ufundishaji na ujifunzaji ziongezeke.

# Polisi yaitaka jamii kutoa ushahidi matukio ukatili

Na Christina Mwakangale

JESHI la Polisi Dawati la Jinsia na Watoto Chang'ombe, Mkoa wa Dar es Salaam, limetoa wito kwa jamii kushirikiana na jeshi hilo kutoa taarifa na ushahidi kuhusu matukio ya ukatili wa kijinsia.

Aidha, limesema kwa wiki moja hupokea kesi takribani 10 na miongoni mwake nane hukosa ushahidi wa kukamilisha upelelezi na kusababisha hatua za kisheria kushindwa kuchukuliwa dhidi ya watuhumiwa wa vitendo hivyo.

Inspekta Blandina Dunguru kutoka Kituo cha Polisi Chang'ombe Dawati la Jinsia na Watoto, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akiwasilisha mada kuhusu ukatili wa kijinsia na kusema kuwa matukio yanayoongoza kuripotiwa kwenye dawati hilo ni pamoja na ulawiti.

"Matukio ya ukatili yanaongezeka ni mengi, ulawiti zaidi. Kwa wiki dawati linapokea kama kesi 10 na hizo ni zinazowahusu watoto wenye umri wa kuanzia miaka 12 hadi 18, achilia mbali ya watoto wenye umri mdogo shule za msingi, yaani chini ya umri wa miaka 12.

"Lakini changamoto ipo katika kukamilisha hatua za kisheria za matukio hayo, ushahidi hakuna. Ukatili wa kijinsia haipiti siku bila kuripotiwa, tukio la unyang'anyi linaweza lisiripotiwe, lakini sio ukatili hasa mimba kwa wanafunzi, ubakaji," alisema Inspekta Blandina.

Aidha, Daktari wa binadamu, Abubakar Rehani, akiwasilisha mada kuhusu afya uzazi, aliwataka vijana kulinda afya zao kwa kujiepusha na ngono zembe, ili kuepuka magonjwa ya zinaa, Ukimwi na mimba zisizotarajiwa.

"Kama wafanyabiashara wadogo au ilivyozoeleka wamachinga, afya yenu ndio kila kitu yaani ni mtaji, kwa sababu kila siku lazima utoke, utembee kuuza bidhaa zako, afya ikitetereka maisha na uchumi wako unayumba," alisema Dk. Abubakar.

Mratibu wa Mradi wa Imarika unaosimamiwa na Shirika la Mulika Tanzania, Winfrida Mponzi, alisema lengo la mradi huo ni kutoa elimu kwa wamachinga kuhusu afya ya uzazi, uongozi, ukatili wa kijinsia na uchumi.

"Vijana 50 wanaojishughulisha na biashara ndogo maarufu wamachinga kutoka Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam, wamepatiwa elimu ya afya ya uzazi, ukatili kijinsia pamoja mbinu za kutafuta masoko.

"Idadi ya vijana hawa inafikisha jumla yao 120 walipewa mafunzo kama hayo Wilaya ya Temeke, ambayo yamefadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA)," alisema.

**"Matukio ya ukatili yanaongezeka ni mengi, ulawiti zaidi. Kwa wiki dawati linapokea kama kesi 10 na hizo ni zinazowahusu watoto wenye umri wa kuanzia miaka 12 hadi 18, achilia mbali ya watoto wenye umri mdogo shule za msingi, yaani chini ya umri wa miaka 12.**



Waliokuwa askari polisi, Ramadhan Tarimo (kulia) na Majidi Abdallah wakiwa wamefunika nyuso zao wakielekea Mahakama ya Kisutu kusikiliza kesi ya unyang'anyi kwa kutumia silaha na kumwibia Grace Mataga Sh. milioni 90. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wataalamu washauri sheria, sera imara biashara ya hewa ukaa

Na Salome Kitomari

WATAALAMU wa nishati wameshauri kuwapo kwa sheria na sera imara nchini zisizobadilika ambazo zitavutia wawekezaji hasa kwenye biashara mpya ya hewa ukaa ili kuhakikisha hadi 2030 miradi mingi ya nishati mbadala inakuja nchini.

Akizungumza hivi karibuni katika mkutano wa Muungano wa wafanyabiashara na wawekezaji Tanzania (TATIC), Mtaalamu wa mabadiliko ya tabianchi wa Shirika la Article 6 Projects Development Afrika, South Pole, Tajiel Urio, alisema hadi sasa asilimia 20 pekee ya fedha za nishati mbadala zimekuja Afrika.

Alisema kwa nchi za Afrika kunufaika na biashara ya hewa ukaa ni lazima kuratibu juhudi, uwapo uwajibikaji na uwazi, ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wananchi wanaotunza misitu inayofyonza hewa ukaa inayozalishwa kwa wingi duniani na nchi zilizoendelea.

Tajieli alisema mwaka 2009 nchi zilizoendelea na zenye viwanda vingi zikizalisha hewa ukaa kwa wingi na kuchangia kuharibika kwa tabaka la juu la anga na kutokea mabadiliko ya tabianchi, zilitangaza kulipa zaidi ya dola milioni 100 kama fidia kwa nchi zilizoathiriwa na mabadiliko hayo ambazo nyingi ni Afrika.

"Mkutano wa wakuu wa nchi wa COP09 uliofanyika Milan, Italia, ulikuwa na matumaini makubwa kwa dunia kupata sauti moja ya mkataba mmoja kuhusu kukabili mabadiliko ya tabianchi, ingawa hawakufikia lengo. Ahadi ya dola milioni 100 ili zitumike kwenye fidia kwa walioathiriwa haijatimizwa hadi sasa," alisema.

Alisema nchi zinazoendelea Tanzania ikiwamo zinazochangia uharibifu kidogo sana na zinatumia bajeti zake kukabili athari za mabadiliko ya tabianchi, huku asilimia 20 ya miradi ya nishati pekee ndio inakuja Afrika.

Tajieli alisema athari za mabadiliko ya tabianchi zinaendelea kuonekana hasa ukanda wa Bahari ya Hindi huku visiwa vya Pangani na Rufiji vikiathiriwa zaidi, vingine 'vikiliwa' na bahari na hivi karibuni huko Pemba maji ya bahari yameingia kwenye makazi na mashamba kwa umbali wa mita 150 na sasa hapafai kwa shughuli za kilimo, visima vya majisafi na huduma za kijamii zimeharibiwa.

Alisema kuelekea COP28 itakayofanyika Desemba 12, mwaka huu, Dubai, ni muhimu nchi za Afrika zikajipanga na kuwa na sauti moja kwenye biashara ya hewa ukaa ambayo wanunuzi wake ni kutoka mataifa ambayo yanachafua mazingira duniani.

Naye mtaalamu wa mabadiliko ya tabianchi kutoka Uganda, Kiiza Africa, alisema licha ya kuwa na vyanzo vingi vya nishati, lakini bado upatikanaji wa umeme kwa nchi za Afrika ni asilimia 48, jambo linalolifanya bara hilo bado kuwa la giza.

Alisema zaidi ya watu milioni 110 Afrika wameathiriwa na majanga ya mabadiliko ya tabianchi, huku hasara ya kiuchumi ikiwa ni zaidi ya dola za Marekani bilioni 8.5 na Afrika ikizalisha asilimia nne ya hewa ukaa.

Alisema asilimia nane ya misitu duniani iko DRC Congo, huku Kenya ikipata zaidi ya asilimia 25 ya mapato yake kutokana na biashara ya hewa ukaa.

"Soko la sasa la kaboni ni Shilingi bilioni mbili litakuwa mara tano ifikapo 2030, asilimia 23 ya uzalishaji wa kimataifa unaotokana na aina fulani ya bei ya mikopo ya kaboni, huku hadi 2021 vibali vyenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 851 vilitolewa," alisema.

Aidha, alisema inakadiriwa kuwa zaidi ya Dola za Marekani bilioni 50 zimetengwa na soko la dunia la hewa ukaa ifikapo 2030.

Kuhusu sheria za kusimamia biashara hiyo, Africa alisema mwaka huu Kenya ilipitishwa muswada wa Sheria ya Mgawanyo wa Mapato ya Hewa Ukaa, Juni mwaka huu pia Malawi ilizindua mpango wa masoko ya kaboni utakaosaidia uwapo wa misitu na kuhakikisha wanapata alama tani milioni 20 za kaboni.

Alisema Gaboni ilikuwa nchi ya kwanza Afrika kupata zaidi ya Dola za Marekani milioni 17 mwaka 2021 zikitokana na hewa ukaa na kwamba hadi sasa wamepata zaidi ya Dola za Marekani milioni 150.

"Nigeria ndio nchi inayonyonya kaboni nyingi na inazalisha alama tani milioni 30 kila mwaka hadi 2030, na kwamba inakadiriwa wanapata mapato ya zaidi ya Dola za Marekani milioni 500," alisema.

Alisema kwa hali hiyo nchi za Afrika zenye misitu mingi zinageuka kuwa 'dampo' la hewa ukaa, "tunakwenda kwenye ukoloni mamboleo katika kujitengenezea njia ya maendeleo na kutengeneza utegemezi wa hali ya juu wa mapato ya hewa ukaa."

Alisema ni muhimu kwa nchi za Afrika kuitazama biashara hiyo kwa jicho la tatu na kuhakikisha maslahi ya nchi zao yanalindwa ili kuepuka kuwaingiza wananchi wake kwenye matatizo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Uchakavu shule wakwamisha wanafunzi kuhudhuria masomo

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

SHULE ya Msingi Kitanga, Kata ya Msimbu, Wilaya ya Kisarawe inakabiliwa na uchakavu wa majengo, hali inayosababisha kipindi cha mvua wanafunzi kusitisha vipindi vya masomo.

Kati ya vyumba sita vya shule hiyo vitano ni vibovu na mvua ikinyesha wanafunzi wanakaa katika chumba kimoja kujikinga.

Hayo yamebainishwa na Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Rhobi Nyamuhanga, wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya mkutano wa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, alioufanya kusikiliza kero za wananchi na kukagua mradi wa ujenzi wa shule hiyo.

Alisema kwa sasa mahitaji ni vyumba vinane vya madarasa na vilivyopo ni sita ambavyo vitano ni vibovu mvua ikinyesha vinavuja na vipindi vya masomo kusitishwa.

Wakazi wa Kijiji cha Kitanga walimwomba Mkuu wa Mkoa huo kusaidia ukarabati kwa baadhi ya vyumba ili wanafunzi hao wasome katika mazingira mazuri.

Elizabeth Johnson, alisema wanafunzi wa shule hiyo kwasasa wanasoma katika mazingira magumu kutokana na uchakavu wa majengo mengi ya shule hiyo huku mwalimu mkuu akilazimika kuhama nyumba kutokana na uchakavu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Beatrice Dominic, alisema shule hiyo imetengewa Sh. milioni 25, na kwamba wahandisi wamefika kuikagua na kubaini majengo yatakayofanyiwa ukarabati na mengine ambayo yatahitaji kubomolewa ili kujengwa upya.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliwasihi wazazi kusimamia elimu kwa watoto wa kike, huku akiwaonya kuachana na mila zinazokwamisha mtoto wa kike kukosa masomo.




Katibu Mtendaji wa Chemba ya Madini Tanzania, Mhandisi Benjamin Mchwampaka, akielezea lengo la warsha maalum ya mafunzo na mwongozo kuhusu ufuatiliaji wa usalama wa mabwawa ya tope sumu na mabwawa ya maji ya kawaida inayotarajia kuanza tarehe 28 hadi 30 Novemba 2023 jijini Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Daraja lililosogezwa na mvua larudishwa mahala pake Tunduru

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, amewaasa wakazi wa vijiji vilivyo jirani na daraja la Mto Mhuwesi, wilayani Tunduru kutunza mazingira na miundombinu ya daraja hilo ili liweze kupitika wakati wote.

Daraja hilo ni kiunganishi kwenye barabara kuu ya kutoka Songea kwenda mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara, Pwani na Dar es Salaam na nchi jirani ya Msumbiji.

Mkuu wa Mkoa, aliyasema hayo jana wakati akipokea taarifa ya urejeshaji wa daraja la Mto Mhuwesi ambalo awali lilikuwa limesogezwa na maji katika kipindi cha msimu wa mvua iliyokuwa inanyesha kipindi hicho na kusababisha mafuriko na barabara kulazimika kufungwa ili kupisha matengenezo ya kulirudisha daraja la zege mahali pake.

Alisema, serikali ilisharidhia kutoa fedha zaidi ya Sh. bilioni 1.55 kwa ajili ya kurejesha sehemu yake daraja hilo baada ya mvua kulisogeza na kwenda sehemu nyingine na kuwa kikwazo kwa wananchi na wafanyabiashara.

Kanali Thomas alisema viongozi wa serikali wilayani humo wanapaswa kuzingatia sheria za mazingira ikiwamo wakulima kufuata taratibu za kibinadamu kufanya shughuli mita 60 kutoka kwenye kingo za mto na kuwaonya watu wenye tabia ya kupita kuchimba madini kando ya mto.

Aliuagiza uongozi wilaya hiyo kuchukua hatua za haraka wanapowabaini watu wanaoharibu miondombinu hiyo.

Aidha, aliwapongeza wataalamu wa wakala wa barabara (TANROADS) nchini pamoja na mkandarasi wa Kampuni ya Mtwivila ya kutoka mkoani Iringa, ambao walifanya kazi nzuri na kufanikisha kulisukuma daraja hilo la zege lenye uzito wa tani 2,000 ambalo lina uwezo wa kupitisha magari yenye uzito zaidi ya tani 100.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Mlima Ngaile, alisema daraja la Mto Mhuwesi awali lilijengwa kupitia mradi wa barabara ya Tunduru Mangaka na Matambaswala yenye urefu wa kilomita 202 kwa kiwango cha lami chini ya ufadhili wa AFDB.

Alisema Februari 14, mwaka jana, kulitokea mafuriko na kujaa kwa Mto Mhuwesi na kufurika katika barabara ya Songea-Tunduru-Mtwara na daraja hilo lilifunikwa na maji na kusambaa umbali wa mita 100 wa pande zote za maingilio za daraja hilo.

TANROADS Ruvuma kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Tunduru, ililazimika kufunga barabara na kuzuia matumizi ya sehemu hiyo kwa kipindi chote cha mafuriko.

Mhandizi Ngaile alisema baada ya kujiridhisha na uimara wa daraja, magari yalianza kuruhusiwa upande mmoja wa barabara ili kuepusha madhara mengine.

Baadhi ya wananchi wa vijiji vya jirani na daraja hilo wameipongeza serikali kwa jitihada za kulirejesha daraja hilo na kuanza kutumika na kushauri kuendelea kuwaamini makandarasi wazawa badala ya kuwapa kipaumbele wa kutoka nje ya nchi.

## LATRA yawataka abiria kusafiri kwa vyombo vilivyokatiwa bima

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imewataka abiria kusafiri kwenye vyombo vya moto ikiwamo mabasi ya kwenda mikoani, pikipiki, bajaji na gari za kukodi zenye bima ili inapotokea bahati mbaya mtu akipata ajali analipwa.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, wakati wa hafla ya kusaini mkataba wa maelewano wa kuboresha huduma za usafiri nchini baina ya mamlaka hiyo na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzaniai (TIRA) na miongoni mwa malengo ni pamoja na kurahisisha taratibu za malipo na kwa wakati kwa wale wanaoathirika na ajali kupitia vyombo vya moto.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, alisema kupitia mkataba huo, wanaamini utarahisisha kuondoa usumbufu kwa waathirika wa ajali na watakuwa wanalipwa kwa wakati tofauti na awali ambapo walikuwa wakicheleweshwa kupata malipo hayo baada ya kuathirika na ajali ya vyombo vya moto.

Pia alisema vyombo vyote vya moto vinavyopatiwa leseni ya kusafirisha abiria na mamlaka hiyo vitalazimika kuwa na bima hiyo.

"Tunawashauri abiria, asikubali kusafiri kwenye gari bila kuhakiki kama ina bima, kabla ya kukata tiketi wajiridhishe kwanza kama gari husika ina bima kwa kuingia kwenye mitandao ya TIRA. Tunasema hivyo kwa sababu endapo ukipanda gari isiyo na bima halafu bahati mbaya ukapata ajali hauwezi kulipwa, lakini yenye bima unalipwa," alisisitiza Suluo.

"Tunaendelea kusisitiza abiria wajitahidi kutunza tiketi zao wanaposafiri kwa sababu ni muhimu linapokuja suala la malipo na kupitia mkataba huu, tunataka kuwawezesha mawakala wa bima ambao wanasimamiwa na TIRA, watoe leseni ya LATRA na hii itamrahisishia msafirishaji mchakato wa kupata bima na leseni ya usafirishaji," alisema Suluo.

Alisema miongoni mwa vyombo vinavyohusishwa katika mkataba huo ni pamoja na vyombo vya moto binafsi na vyenye miguu mitatu (boda na bajaji).

Kamishna wa Bima kutoka TIRA, Dk. Baghayo Saqware, alisema ushirikiano huo utajikita katika nyanja mbalimbali ikiwamo elimu kwa umma, kurahisisha upatikanaji wa taarifa za watoa huduma na kuwawezesha mawakala wa bima nchini kutoa leseni za usafirishaji.

"Tunaamini ushirikiano kati ya taasisi hizi mbili utaleta faida nyingi kama vile kurahisisha ufanyaji kazi na upatikanaji wa huduma, pia itarahisisha utoaji wa elimu kwa Watanzania na kuongeza uelewa kwa wadau," alisema Dk. Saqware.



## Walimu darasa la awali wapigwa msasa utoaji elimu bora

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WALIMU 40 wa darasa la awali wilayani Babati mkoani Manyara, wamepewa mafunzo ya kuwawezesha kutoa elimu bora ya kuwaandaa wanafunzi kujua kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK), wanapoanza darasa la kwanza.

Ofisa Elimu kutoka Shirika la World Vision Tanzania, Akaunsia Munuo, akizungumza na Nipashe jana alisema wameanzisha kambi ya kusoma watoto wadogo kwenye vijiji.

"Tunaanzia darasa la awali tunahakikisha madarasa yana zana za kufundishia na zana hizo hazina gharama zinapatikana kwenye mazingira ya wanafunzi wanakotoka," alisema Munuo.

Aidha, alisema wana walimu maalum waliosomea kufundisha elimu ya awali na wanaofundisha KKK.

Alisema walipoanzisha utaratibu huo walikuwa wanachukua walimu wa shule za serikali na walimu kutoka kwenye jamii wanawakutanisha pamoja na kuwapa mbinu za kuwafundisha wanafunzi wa awali.

Vilevile, alisema kukosekana kwa walimu wa awali ni chanzo cha wanafunzi kushindwa kusoma, kuandika na kuhesabu.

Mshauri wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto kutoka Shirika la Children Incrossfire (CIC), Davis Gisuka aliiomba serikali kuwekeza kwa walimu wa awali ili kuondoa tatizo la uhaba wa walimu wenye ujuzi wa kufundisha elimu ya awali.

Ofisa Elimu Mkoa wa Manyara, Halfan Masukira, alisema kila shule ya msingi ina darasa la awali na yupo mwalimu anayefundisha wanafunzi hao.

Kwa upande wake mkazi wa Kijiji cha Magugu, Iddy Haji alisema uwepo wa walimu wa awali ni kichocheo cha wanafunzi kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na kuwarahisishia wanapopanda darasa kuwa na uwezo wa kumudu lugha.

Kwa mujibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT- MMMAM) ya mwaka 2021/22-2025/26 inaeleza kuwa kuna upungufu wa walimu wa elimu ya awali ambapo wengi wao wana ujuzi wa elimu ya msingi na siyo elimu ya awali.

PJT-MMMAM inafafanua kuwa mwaka 2018 Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia iliripoti upungufu wa asilimia 31.7 ya walimu wa elimu ya awali wenye vigezo katika shule za serikali kutoka walimu 7,861 mwaka 2017 mpaka walimu 5,367 mwaka 2018.

# Wataalamu: Uchumi wa Tanzania unakua kwa kasi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WATAALAM wa masuala ya kiuchumi wamesema uchumi wa Tanzania unakua kwa kasi ukilinganisha na wa nchi ya Afrika Kusini kutokana na kuwepo kwa fursa mbalimbali za uwekezaji kwenye sekta za viwanda, biashara na kilimo.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Mtaalam wa Uchumi, Dk. Cairo Mwaitete, wakati akizungumza kwa niaba ya wataalamu wengine wa uchumi wakati wa mkutano wa uchumi shirikishi kwa jamii ili kuhamasisha vijana waweze kulinda na kunufaika na uchumi wao.

Alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na fursa nyingi, hivyo wageni wanakuja kuwekeza kwenye sekta mbalimbali.

"Pamoja na ukuaji wa uchumi wetu unaokwenda kwa kasi kwa asilimia saba kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita kwa nchi yetu ya Tanzania ukilinganisha na ule wa nchi ya Afrika Kusini bado tunatakiwa kuwaandaa vijana ambao wataweza kuanzisha viwanda na biashara kubwa.

"Hapa nchini kuna fursa nyingi mno kwenye maeneo ya malighafi, viwanda, uchimbaji wa madini na kilimo hivyo tunataka kuona Watanzania wanamiliki mashamba makubwa na kulima, tunataka kuwaone watu wetu wakichimba na kuuza madini nje ya nchi pamoja na kuanzisha viwanda vikubwa kwa kuwa Watanzania wana uwezo, hivyo wahusika wanapaswa kuangalia sera zetu," alisema.

Vilevile alitoa rai kwa watunga sera kutunga sera ambazo zitakwenda na wakati hasa kwa kuangalia mazingira ambayo yanahitaji mashirika na taasisi binafsi ziweze kusimamiwa na Watanzania wenyewe badala ya watu kutoka nje ya nchi.


"Niaomba watunga sera kupitia na kuangalia sera ziwe za ushirikishaji wa kijamii wa uchumi shirikishi ambao utaleta matokeo kwa mtu mmoja mmoja ili kuongeza pato la taifa.

"Lengo la mkutano huu ni kuwahamasisha vijana kujifunza namna ya kuingia kwenye uchumi na wawe na ujasiri hata wa kuanzisha viwanda, biashara kubwa na kuingia kwenye kilimo na kutambua fursa zinazoizunguka nchi ya Tanzania," alisema.

Mkurugenzi wa Utafiti, Ushauri na Machapisho kutoka Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Dk.Mordecai Matto alisema katika mkutano huo wamekutana na wadau kujadiliana namna ya kufikia uchumi shirikishi na changamoto zinazowakabili katika jamii.

"Uchumi unaopendwa kwa sasa duniani ni ule ambao unashirikisha watu wote katika nchi, hivyo sisi wataalam wabobezi wa masuala ya uchumi tumejadiliana mambo mengi na wadau ili kufikia malengo ya kuwa na uchumi shirikishi," alisema Dk.Matto.

Alisema kwa sasa utafiti nyingi zinazofanyika duniani zinajikita zaidi kwenye uchumi shirikishi unaogusa watu wote kwa kuwa maendeleo yasipomfikia mtu mmoja mmoja kunakuwapo kwa changamoto kwenye nchi.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake (UWT) wa CCM Wilaya ya Babati Mjini mkoani Manyara, Eva Makilagi Luoga (kulia), akizungumza na wasichana wa Shule ya Sekondari Kwaang'w, baada ya kuwakabidhi taulo za kike 150 kama zawadi ya kuadhimisha siku yake ya kuzaliwa juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# SFU yaingia makubaliano ya ushirikiano na vyuo vinne

**Na Allan Isack,** ARUSHA

CHUO Kikuu cha Simon Fraser (SFU), kilichopo nchini Canada kimesaini makubaliano ya ushirikiano wa kufanya utafiti wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi na vyuo vinne hapa nchini.

Vyuo vilivyoingia makubaliano na SFU ni Chuo cha Aga Khan, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST).

Akizungumza jana jijini Arusha baada ya utiaji saini saini wa makubaliano hayo, Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Prof.Adolf Mkenda, alisema sehemu kubwa ya ushirikiano huo ni kuendeleza utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi na sayansi kwa ujumla.

Waziri Prof.Mekenda, alisema jambo hilo ni muhimu sana hasa kwenye kusongeza mbele sayansi na teknolojia hususani kwenye sekta ya kilimo ambayo inaathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema Serikali itatoa ushirikiano kwa chuo cha Aga Khan ili waweze kuwa na chuo kikuu hapa nchini.

"Nimewaomba Aga Khan ikiwezekana waanzishe shule kuu kwa ajili ya mambo ya 'akili bandia' ambayo itakuwa ni ya kimataifa kwa kuwa walimu na wanafunzi watatoka maeneo mbalimbali duniani," alisema.

Rais wa Chuo cha Aga Khan, Suleiman Shahabuddin, alisema wamefurahi hatua ya kuingia kwenye makubaliano hayo kwa kuwa itasaidia kwenda kujikita kwenye kufanya utafiti.

"Dhumuni la kuingia makubaliano hayo ni kwenda kujikita zaidi kwenye suala la mabadiliko ya tabianchi kwa kuchukua hatua ya kukabiliana nayo kwa kuwa jambo ili kila siku limekuwa ni mada inayozungumziwa kila mahali duniani, "alisema.

Naye Rais wa SFU, Dk.Joy Johson, alisema amefurahi kufika Tanzania kwa ajili ya hafla ya utiaji sahini wa makubaliano hayo kwa kuwa suala la mabadiliko ya tabianchi limekuwa tatizo kubwa hivyo kuna umuhimu wa kufanya kazi kwa pamoja.





# Shughuli za binadamu zaharibu hekta 15,000 za hifadhi

**Na Renatus Masuguliko,**
GEITA

HEKTA zaidi ya 15,000 za Hifadhi ya Msitu Lwamgasa uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita mkoani hapa zimevamiwa na kuharibiwa na shughuli za kibinadamu ikiwamo kilimo, uchomaji mkaa, ujenzi pamoja na uchimbaji madini.

Hifadhi hiyo yenye ukubwa wa hekta 28,000 imekuwa ikiharibiwa siku hadi siku hususani na wachimbaji madini ambao wanakata miti kwa ajili matimba ya kuweka katika maduara.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Huduma ya Misitu (TFS) Wilaya ya Geita, Sandusy Ngunyale alitoa taarifa hiyo kwa Mkuu wa Wilaya hiyo kufuatia mpango wa upandaji miti shirikishi ili kurejesha ikolojia yake.

Ngunyale alitaja shughuli nyingine zinazosababisha uharibifu huo kuwa ni pamoja na ukataji miti kwa ajili ya uchomaji mkaa, upasuaji mbao pamoja na uandaaji wa mashamba kwa wakulima.

Alisema serikali imeanzisha mpango huo wa upandaji miti ikilenga kuutekeleza katika hekta zaidi ya 10,000 ambapo kwa awamu ya kwanza watapanda katika hekta 213 ikitarajia kuwa endelevu kwa awamu tofauti.

**Hifadhi hiyo yenye ukubwa wa hekta 28,000 imekuwa ikiharibiwa siku hadi siku hususani na wachimbaji madini ambao wanakata miti kwa ajili matimba ya kuweka katika maduara.**

Aliwataka wanaofanya shughuli za kilimo cha mazao ya muda mrefu ndani ya hifadhi hiyo kuacha mara moja huku wanaofanya kilimo cha muda mfupi watashirikishwa katika mpango huo ili kufanya shughuli zao wakilinda miti inayopandwa.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Corneli Magembe aliwataka wananchi wanaotumia msitu huo kwa kilimo cha muda mfupi kuwa tayari pale watakapohitajika kuondoka hifadhini kufanya hivyo haraka ili kuwezesha mpango huo kufanikiwa.

Diwani wa Kata ya Lwamgasa, Doto Kaparatus alikiri uwepo wa tatizo hilo na kueleza kuwa limetokana na ongezeko la watu kutokana na shughuli za uchimbaji madini wanaofikia zaidi ya 2,000.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda (kulia), akisogeza ndoo baada ya kuzindua mradi wa maji wa vijiji vya Bulinga hadi Busungu katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma juzi, ambao utahudumia wananchi wa vijiji hivyo, vikiwamo vya Bukima na Rusoli. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# COWSO yakabidhiwa pikipiki kusimamia miradi ya maji

**Na Timothy Itembe,**
TARIME

CHOMBO cha Watumiaji Maji (COWSO) cha Mji wa Nyamongo wilayani Tarime kimekabidhiwa pikipiki mbili za Sh. milioni 6.6 na Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa ajili ya kusaidia kusimamia, kutunza na kukarabati miradi ya maji katika eneo hilo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi pikipiki hizo, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Tarime, Malando Sadima, alisema pikipiki hizo zimenunuliwa kwa fedha za mfuko wa uwajibikaji kwa jamii inayotokana na mgodi wa dhahabu wa Barick.

Meneja huyo alisema lengo la matumizi ya pikipiki hizo ni kwa ajili ya mafundi sanifu wanaofanya shughuli za ukarabati wa miradi hiyo pindi inapopata hitilafu na siyo kwa ajili ya wenyeviti wa vyombo hivyo na kuwataka kuzitumia kwa malengo yaliyokusudiwa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Michael Mtenjele, aliagiza miradi hiyo kukaguliwa kwa wakati na kuhakikisha inafanyiwa matengenezo ipasavyo ili kudhibiti ukosekanaji wa maji.

Aidha, aliwataka wote wanaojaribu kukwamisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa lengo la kuihujumu kuacha tabia hiyo mara moja kwani wamejipanga kuwachukulia hatua za kisheria wote watakaobainika katika hujuma hizo.

Diwani wa Kata ya Matongo, Godfrey Kegoye, alisema kuwa kwa sasa utaratibu wa wananchi kuchangia huduma ya maji haujakaa vizuri na kuahidi kuliwasilisha katika vikao vya halmashauri kupanga namna bora ya watumiaji kuchangia.

Aliongeza kuwa mradi huo umewafikia hivi karibuni ukigharimu zaidi ya Sh. milioni 900 na kueleza kuwa watahakikisha wananchi wanachangia huduma hiyo ipasavyo ili kusaidia shughuli za uendeshaji mradi.

Awali akitoa taarifa ya utolewaji huduma ya maji, Mwenyekiti mradi wa maji Nyamongo, Dotto Mang'era alisema jamii haitaki kuchangia gharama za uchotaji maji licha ya kuwa serikali imewapunguzia kutoka Sh.200 kwa doo hadi Sh. 100 kwa ndoo tatu sawa na Sh.30 kwa ndoo moja.

# TANROADS yaanza kutekeleza agizo la Makamu wa Rais

**Na Shaban Njia,** KAGERA

WAKALA wa Barabara Tanzania (TANROADS) Mkoa wa Kagera, umeanza kutekeleza agizo la Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango la ukarabati na upanuzi wa njia nne ya Barabara ya Bukoba Mjini (Rwamishenye-Mzunguko) hadi Bandari.

Dk.Mpango alitoa agizo hilo Machi, 2022 baada ya kupokea kilio cha wananchi juu ya ufinyu pamoja na uwepo wa mteremko mkali katika barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 5.1 unaosababisha ajali za mara kwa mara.

Kaimu Meneja wa TANROAD Mkoa wa Kagera, Mhandisi Ntuli Mwaikokesya akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya barabara kwa waandishi wa habari alisema Sh. bilioni 337 zimetumika kwenye ujenzi wa kilometa 1,966.29 za barabara mkoani humo ukiwamo mradi huo.

Alisema katika eneo hilo kila mwaka zimekuwa zikitokea ajali kuanzia tatu mpaka tano hususani kwa waendesha pikipiki na kueleza kuwa tayari wamelipa fidia ya Sh.bilioni 1.8 kwa kaya 25 zilizofuatwa na mradi huo.

"Tumepokea Sh. bilioni 4.641 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilometa moja ambayo ni njia nne na anayetekeleza mradi huu ni mkandarasi Abemulo Construction Co.ltd na unatarajia kukamilika Oktoba 2024," alisema Mwaikokesya

Alisema kwa sasa kazi inayofanyika ni uondoaji wa miundombionu iliyopo kwenye hifadhi ya barabara kama vile mtandao wa maji wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Bukoba (BUWASA), Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)

"Hivi karibuni tumepokea pia maelekezo ya Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, tuanze ujenzi awamu ya pili kilometa 0.6 ili ifike mjini kati na kufanya usanifu wa njia nne eneo la Kagondo hadi Rwamashinye yenye kilometa tatu," alisema.



Mkazi wa Bukoba Mjini, Adelina Sebastiani alisema kwenye eneo lake la biashara alikuwa ameshawekewa alama ya kuondoa duka lake tangu mwaka 2000, hivyo anajiandaa kuondoka ili asiwe kikwazo cha kukwamisha ujenzi.








Ukurasa 12

TAMASHA LA 15 la JINSIA TANZANIA... Harakati hazifanikiwi bila fedha ndivyo wanawake wanavyowapasha wahisani

Nipashe
TESA
Jumanne Novemba 14, 2023
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




Ukurasa 14

## Kuacha 'CPA' kujiajiri, kuwafunza wanawake sanaa ya sanamu za keki

ELIMU
NA SABATO
KASIKA

DARASA LA CWT WALIMU WASTAAFU...

# Linapowaibulia 'vifurushi' vichochea maisha magumu, unyonge, umaskini

KUKOSA maarifa ya jinsi ya kutumia mafao, elimu ya biashara, ujasiriamali na mmomonyoko kimaadili hasa starehe na 'nyumba ndogo' uzeeni ni baadhi ya vitanzi vinavyonyonga waastafu.

Katika hatua hiyo, kilio cha wengi ni ugumu wa maisha, kukosa maarifa ya jinsi ya kutumia mafao na elimu ya biashara.

Mazingira hayo yanakigusa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Mkoa wa Mara, ambacho sasa huwaingiza darasani walimu wanaotarajia kustaafu miaka mitano ijayo kuwapiga msasa.

CWT inaeendesha mafunzo yanayowashirikisha walimu na watumishi wengine wa ofisi ya mkuu wa mkoa ili kuwaweka sawa wanapostaafu wasikumbane na changamoto ya maisha.

Suzan Shesha ni Katibu wa CWT Mkoa wa Mara, anayesema chama kimekuwa kikipokea changamoto za walimu wastaafu.

Anaeleza hayo anapozungumza na Nipashe."Tumefuatilia chanzo chake tukagundua kuwa zinatokana na sababu nyingi kama kukosa elimu ya biashara na ujasiriamali," anasema Suzan.

Aidha, anawataja baadhi ya wastaafu hukimbilia kufanya biashara bila kuwa na uzoefu, ujuzi hata fedha za kutosha na kukwama.

Anatoa mfano kuwa wapo wanaonunua magari ya biashara lakini wakikutana na kikwazo, mfano fedha za kuyaendesha na wakati mwingine magari ni mabovu yanaharibika mara kwa mara wanakwama.



Katibu wa CWT Mkoa wa Mara, Suzan Shesha (kulia) na wadau wengine wakiwa kwenye semina. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

"Lakini pia wastaafu wanaume, wakishapata mafao wanakumbuka zaidi wanawake. Wengine huongeza wanawake, wapo wanaotafuta vibinti na kutumia mafao kwa starehe, katika mazingira hayo fedha za pensheni lazima ziishe," anasema.

Anatolea mfano mstaafu mmoja aliibiwa Shilingi milioni 15 na binti wakiwa kwenye nyumba ya wageni.

Suzan anaongeza kuwa baadhi ya wastaafu wanawake, huwaamini vijana wao na kuwapa kadi kuwatolea fedha ambao mwishowe huwaibia na kufanyia starehe au matumizi 'mabovu' na wastaafu hao wakibakia na maumivu hata magonjwa ya shinikizo la damu na kuendelea kuteseka kwa sononа.

Wengine wakati wakisubiri mafao huwa wanakwenda kukopa fedha kwa wakopeshaji wenye riba kubwa na masharti ambayo husababisha pale wanapopokea fedha sehemu kubwa wanalipa madeni baada ya kukabwa koo na kausha damu.

"Mazingira hayo ndio ambayo yametufanya tuwe na semina ambayo wastaafu watarajiwa tumewafundisha mambo mengi ili wanapostaafu wawe makini na fedha zao." Susan anaongeza.

### MAELEKEZO

Katibu huyo anasema kuwa katika semina hiyo, walimu walelekezwa kuwa makini na fedha za mafao yao na kwamba wanapozopokea watulie kwanza na kutafuta watu makini wa kuwasaidia kufanya shughuli zenye mafanikio

"Walimu pia tumawashauri kujipanga kuanzia sasa ili kufikia miaka mitano ijayo wawe wanajua ni nini watakachofanya baada ya kustaafu na sio kuvamia biashara ambayo hawana uzoefu nayo," anasema.

Anaeleza kuwa uzoefu unaonyesha wengi wao huamua kufanya shughuli yoyote ambayo hawakuwahi kuifanya na kujikuta wakimaliza mitaji na kibaki hawana kitu.

Kwa ujumla ni kwamba, sababu zote ambazo zinachangia wastaafu wanakuwa hoi baada ya utumishi, zimewekwa wazi, hivyo waliopo kazini wamefundishwa kujipanga kuanzia sasa kila mmoja aone ni shughuli gani anaweza kuifanya baada ya kustaafu ili aanze kuifanyia mazoezi mapema," anasema.

Mwalimu mstaafu, Livingston Gamba, anasema suala la nidhamu ya fedha ni la muhimu na kwamba likizingatiwa linaweza kuwasaidia wastaafu kuishi maisha mazuri.

"Kama ni kujenga nyumba mwalimu anaweza kutumia milioni 30 akatunza milioni 70, kwa ajili ya kuendesha maisha yake. Msisitizo wangu ni nidhamu ya fedha," anasema Gamba.

Anaongeza kuwa ana miaka miwili tangu astaafu na kwamba anaendesha maisha kama kawaida kupitia biashara ya kuuza mbao ambayo aliijaribu mapema kabla ya kustaafu.

### WASIO WA RC

Katika semina hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda, ndiye alikuwa mgeni rasmi na anawataka wastaafu watarajiwa kuanza mapema maandalizi ya kustaafu.

"Ni muhimu kufanya maandalizi mapema, ili baada ya kustaafu maisha yaendelee kama kawaida, hivyo ni vyema mkubaliane na ukweli kwamba mnakwenda kustaafu na muanze kujipanga kwa ajili ya kujua cha kufanya nje ya utumishi wa umma.

ELIMU
NA MWANDISHI
WETU

# Harakati hazifanikiwi bila fedha ndivyo wanawake wanavyowapasha wahisani

• Wapinga mashirika kupewa pesa kiduchu, ufadhili wenye vikwazo na sura ya ukoloni

BAJETI na kupatikana fedha za kutosha kwa mashirika yanayotetea haki za wanawake na watoto ili kuleta mabadiliko ni suala linalotazamwa kwa jicho la tatu na wadau wanaharakati za ukombozi wa mwanamke kimapinduzi (feminism), wakihoji ziko wapi fedha kwa ajili ya kufanikisha mipango na kufikia maendeleo kiusawa?

Jijini Dar es Salaam, linafanyika Tamasha la 15 la Jinsia Tanzania na maadhimisho ya miaka 30 ya Mtandao wa Jinsia (TGNP), mengi yakizungumzwa na suala la ufadhili wa kazi za harakati za ukombozi wa wanawake ili kuufikia usawa kijinsia likipewa uzito na mikakati ya kufanikisha upatikanaji wa fedha zaidi.

Rose Marando ni Mkurugenzi wa Mfuko wa kutoa ruzuku kwa mashiriki ya utetezi wa haki za wanawake kwenye ngazi ya jamii (WFTT), anazungumzia kwanini suala la fedha za ruzuku linahitaji kipaumbele ili kupata fedha za kutosha kufikia malengo ya kubadilisha jamii kazi inayofanywa na wanawake kwa kiasi kikubwa.

Anasema harakati zinahitaji fedha ili kufanikisha kampeni mbalimbali kama lishe, tiba na elimu bora, ushiriki na ushirikishwaji na kuwa sehemu ya kufikia na kupata maendeleo ngazi za jamii na taifa.

Ili kutimiza azma hiyo wanawake wanahitaji ruzuku, misaada au fedha kufanya harakati zinazoleta mabadiliko, lakini taasisi za kifeminia hazipewi fedha zakutosha kufanya kazi hizo anasema Rose.

Katika moja ya semina zinazofanyika wakati wa tamasha hilo, kujadili upatikanaji na hali ya fedha, anawaambia washiriki kuwa mashirika makubwa yanayotoa fedha ziwe za uhisani binafsi na misaada na ruzuku kwa nchi zinazoendelea hasa za kusini - Afrika Kusini ya Sahara na Asia zinazowafikia wanawaharakati wanawake ni kiduchu mno.

Anasema ni chini ya asilimia moja ya mabilioni yanayotolewa na kwamba ni kama 'tone' hufikia mashirika hayo ya kiharakati yanayoshughulikia kutetea haki za wanawake na watoto.

Anasema pamoja na udogo, fedha hizo zimewekewa vikwazo ili kuendeleza misingi ya mifumo kandamizi ya kiuyonyaji na hata ya kiubaguzi wa baadhi ya makundi kwenye jamii na mataifa pia.



Baadhi ya washiriki wa Tamasha la Jinsia 2023. **PICHA ZOTE: MWANDISHI WETU**

> Fedha zinakuja kidogo lakini kinyume na vitu ambavyo wafeminia (wanawake wanaharakati) wameviona na kuvifanyia kazi na kuleta mabadiliko.

Halikadhalika zinaambatana na vigingi vinavyopingana na kazi na mipango ya wafeminia, huongeza mgwanyiko wa harakati zao na kuleta ushindani badala ya ushirikiano.

"Ukitaka kufanya kazi za kutetea wanawake usiwagawanye, wanachotaka ni maji, afya ya uzazi, lishe na elimu bora, ajira zenye staha. Hakuna tofauti. Lakini wanaotoa fedha kwani ni kidogo na wanawagawanya wanawake. Mfano wanataka zishughulikie kundi dogo na changamoto moja , wanasahau kuwa wafeminia wanasema mabadiliko yanachukuliwa kwa ujumla wake. Hivyo kuleta fedha kidogo kwa ajili ya 'kamradi kadogo kwa miezi michache au mwaka mmoja si jambo jema kwenye juhudi za wanaharakati,"anaonya Rose.

Anawaambia washiriki kuwa fedha pia huletwa kwa masharti yanayowagawa wanawake. Wahisani wakijua kuwa wameshajiunga kwenye movement 'tapo la wanawake' wanatoa fedha kimakundi badala ya kuleta nguvu za pamoja katika ufeminia.

Anafafanua kuwa masharti na mgawanyo vinaonekana kwenye kutakiwa kwanza kushindana kwenye kuandaa andiko, maana kabla ya kuzipata wanalazimika kuwasilisha andiko (proposal) inayoweza kukubaliwa au kutupwa. Wanalazimika kutumia muda na gharama kubwa kuandika taarifa za mradi, kueleza ulikwenda je, tathmini badala ya kuangalia vipaumbele vimetimia kama mabadiliko yaliyokuwa yanalengwa yamepatikana kwenye afya ya uzazi, sheria zinazokinzana zilizorekebishwa na mabadiliko ya watu.

"Fedha zinakuja kidogo lakini kinyume na vitu ambavyo wafeminia (wanawake wanaharakati) wameviona na kuvifanyia kazi na kuleta mabadiliko".

Aidha, anasema ruzuku, fedha na misada zinakuja kwa uchache na udogo lakini hazibebi ajenda ya kile mwanamke anachohitaji au ajenda yake, badala yake zina ajenda za wahisani au mtoa ruzuku, akieleza kuwa ni mambo yanayohitaji kufanyiwa mabadiliko sasa.

"Ni lazima mabadiliko na ajenda yatoke kwenye jamii yenyewe siyo ya kushusha kutoka juu.

### CHA KUFANYA

Rose anayaambia mashirika ya kifeminia kuwa cha kwanza ni wanaharakati nchini kupaaza sauti tena kwa kujiamini wakijua kwamba kama waliweza kubadilisha mifumo kandamizi na kuleta hali bora ya mwanamke ni lazima tena zije sauti za pamoja za kupiga kelele ili fedha zije na zitolewe kwenye maeneo ambayo ndiko kilipo kitovu cha kuleta na kufikia mabadiliko ya kweli.

"Tunasema zije za kutosha na kubadilisha mifumo kandamizi siyo kiduchu bali kwa kuwezesha kufumua chanzo cha matatizo na kufanya marekebisho ya hali za watu wetu.

"Kingine cha kutusaidia ni kufanya utafiti.Tuje na ripoti za tafiti nasisi WFTT tunataka tuzifanye, zitakazotuonyesha uhalisia wa hali halisi ya Kitanzania. Kwa sababu hata tunapoongea habari zetu, tunarejea na kutumia ripoti za utafiti za wenzetu Afrika. Hapa nyumbani nasi tuangalie fedha ziko wapi? Ni kiasi gani, zinakujaje? zinatoka wapi, zinakwenda wapi?... ili tutakapoanza kufanya uchechemuzi (advocacy) tuweze kujua ukweli na tuhakikishe kuwa tunapata fedha za kutosha zinazofanikisha kupata mabadiliko," anasisitiza.

Anaongeza kuwa ni lazima pia utafiti ujibu fedha zinakwenda wapi na zinatolewa na taasisi zipi , hata hizo zinazotoka kwa wahisani wa ndani na ruzuku za serikali ili kufanya maboresho na sera na sheria.

### UHISANI KIJAMII

Anaugusia uhisani wa kijamii (social philanthropy), ambako watu huchangia harusi, sherehe mbalimbali, kusomesha wanandugu na hata kujenga makanisa uhisani ukitumia mamilioni ya fedha.

"Kwa wahisani wa kijamii wa nchi zilizoendelea wanatoa fedha ili kupunguziwa kodi na serikali zao lakini kwa Watanzania imekuwa ni sehemu ya maisha yetu, tunasomesha watoto wa ndugu, tunachangia harusi, vyama, kujenga makanisa na taasisi nyingine ni sawa. Lakini sasa tufikikirie kujenga mifuko mingi ya uhisani kwenye jamii (community phillanthropy) zenye kule tija ya michango yetu ili tufikie maendeleo makubwa zaidi."

Anataja mfano kuwa mtu anaweza kuchangia hata 800,000 kwenye harusi au mamilioni kusomesha ni vyema kuwa na mifuko ambayo italeta matokeo na mafanikio makubwa zaidi kwasababu Watanzania wanaweza na wamethibitika kuwa wanaweza kuchangia na kufanikisha maendeleo yao.

"Tujenge mifuko na mifumo ambayo imesimama isiwe inayojijenga na kukua zaidi na zaidi na kujiletea maendeleo makubwa zaidi na si kuacha mambo yabaki kama yalivyo sasa."

### SEKTA BINAFSI

Mkurugenzi wa WFTT anaelezea umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi kwenye kutoa fedha na uhisani kwa wanaharakati wa kifeminia, akisema ni wakati wa kujenga daraja ambalo litasaidia wafanyabiashara hao kuwafikia Watanzania na jamii kwa biashara zao.

Kazi na taarifa zao zifanikishe harakati za wanawake kwa mfano kuwa na fuko la pamoja (pool fund), zitakazogawanywa na kufikia watu wengi zaidi badala ya kuangalia kile wanachorudisha kwa jamii (CSR) .

Wanatoa kuchangia maendeleo ya jamii ni sawa lakini wanaweza kuangalia namna ya kuunda mfuko kama ilivyo kwa wafanyabiashara wengine mfano Ford Foundation , Master Card Foundation na kujenga mifuko ambayo inaleta maendeleo makubwa kwa taifa, anashauri Rose.

"Sawa wanafanya juhudi kuchangia urembo, mpira, marathon...lakini wanaweza kulete na kuacha alama zaidi mfano kampuni inaweza kujivunia kuwa ilipouza bidhaa sikuuza tu lakini ilisaidia wana jamii kufikia maendeleo makubwa kwenye elimu, afya na mazingira bora kupitia kazi zilizofanywa na harakati za wanawake ."

### WIZARA YA FEDHA

Rose anagusia pia fedha kutoka serikalini, akitaja fedha za halmashauri zinazotolewa asilimia nne kwa kinamama, mbili kwa wenye ulemavu na nne kwa vijana akisema fedha hizo sasa zimesimama zikifanyiwa michakato ya namna ya kuzitoa upya.

Anashauri taratibu zitakazofanyika zisilete vikwanzo wala ugumu wa kuzipata au kuwakwamisha na kuwarudisha wanawake nyuma au chini kwenye kujilete maendeleo.

Anapendekeza utaratibu uwe rafiki na kuwezesha kufikia walengwa kuanzia mwanamke, mwenye ulemavu, au wasio na uelewa , vijana ili fedha ziwafikie wanaolengwa na kutimiza malengo na kupata mabadiliko.




Hanifa John, akizungumzia ruzuku ya 4:4:2.

### AFRIKA MOJA

Francis Kiwanga ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi wa Foundation for Civil Society, anasema ili kupata fedha na ruzuku kwa ajili ya maendeleo, anasema ni lazima sasa Afrika kuwa na sauti moja.

Anasema wanaharakati wa Afrika wanazungumza lugha moja na kupinga mifumo kandamizi ya utoaji fedha ambao haulengi kubadilisha hali mbaya na kuinua maisha ya watu .

Anasema wanaharakati na asasi za kiraia za Afrika wamejiunga pamoja na kuanzisha ajenda inayoitwa 'shift the power', inayomaanisha kuwa mashirika na mitandao mbalimbali inakataa Afrika kuletewa ajenda na masuluhisho na maelekezo kutoka nje, badala yake kutoa maoni na maelekezo yao pia kwa imani kuwa ushirikishwaji na kusikilizana vinawezekana.

Anasema juhudi za kujipatia uhisani wenye tija na unaosaidia kuleta maendeleo zinafanywa na mtandao wa Africa Phillanthropy Netwok ili kupata mabadiliko na kupigania fedha zije zaidi.

Hata hivyo anasisitiza kuwa fedha zinazotolewa bado zina sura ya kiukoloni kwa mfano fedha zinazotolewa zinaweza kuongeza na kupeleka zaidi mizigo kwa wananchi na hilo ni jambo ambalo sauti za pamoja zinatakiwa ili kulipunguza.

> Mwenye ulemavu mfano matatizo ya akili hawezi kuomba fedha ila anayemhudumia, lakini wanawake wengi hawafahamu na inakuwa vigumu ruzuku hiyo kuwanufaisha.

Anasema kuna wahisani walitaka fedha walitaka kutoa fedha kupitia kwenye taasisi binafsi lakini kwa umoja wao wamekataa na kuhoji inakuwaje mmoja anafanya kazi kwa mrango usio wa kihisani na mingine wa kutengeneza faida wakashirikiana?

Kiwanga anasisitiza umuhimu wa kushirikiana na kubadilisha mifumo na ikiwezekana kupata fedha kwa wingi bila kukandamiza mashirika ya nchi maskini.

### 4:4:2 YALALAMIKIWA

Licha ya serikali kutoa ruzuku kusaidia wanawake na vijana wote wakipata asilimia nne na wenye ulemavu asilimia mbili (4:4:2) katika Tamasha la Kijinsia mwaka huu, wenye ulemavu wamekosoa unyanyanyapaa baadhi ya wenye ulemavu wanaokutana nao.

Hanifa John ni mama wa mtoto mwenye ulemavu na matatizo ya mifumo ya fahamu na akili, anazungumza kwenye semina hiyo ya masuala ya fedha, akisema kuwa utoaji wa ruzuku ya halmashauri unawaumiza wenye mahitaji maalumu.

Anasema alikwenda kwenye halmashauri (jina tunalo) kuomba fedha za fungu la asilimia mbili za wahitaji na akapokelewa kwa kufukuzwa, akiambiwa 'ondoka una ulemavu gani wewe.'

Anawaambia washiriki kuwa inasikitisha kwa sababu mtu mwenye ulemavu mfano mtindio wa akili hawezi kuomba fedha inabidi anayemhudumia aombe ruzuku kufanya mradi kupata fedha na kumtunza lakini ni ajabu wengi hawalifahamu hilo hata viongozi wa halmashauri wanaoshughulikia mikopo.

Hanifa anasema mwenye ulemavu mfano matatizo ya akili hawezi kuomba fedha ila anayemhudumia, lakini wanawake wengi hawafahamu na inakuwa vigumu ruzuku hiyo kuwanufaisha.

Anashauri kufanyike hamasa na kuelimisha jamii zinazotunza watoto na jamaa zao wenye ulemavu ili waombe ruzuku hiyo, waanzishe biashara na miradi ya kiuchumi kulisaidia kundi hilo, badala ya kukaa kimya, kuwafokea na kuwafukuza kama ilivyotokea kwake.

Anasema kukosa uelewa, taarifa na ufahamu kuhusu ruzuku hiyo kunakwamisha wanawake maskini kutumia fursa na kujikwamua na kuwasaidia wahitaji wanaowalea, akitoa mfano:

"Ukipata ruzuku unaanzisha biashara, unamsaidia mwenye matatizo kwa kununua dawa inayompunguzia maumivu wale wasiofahamu hawawezi kupata tiba watoto wanazidi kuumia. Ukiwapa tiba inapunguza tatizo," anasema Hanifa.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

SCOLASTICA SULTAN, SIJUTI

# Kuacha 'CPA' kujiajiri, kuwafunza wanawake sanaa ya sanamu keki

HUYU ni msomi mhasibu mwenye shahada ya juu ya uhasibu (CPA), ambaye ujasiriamali na ubunifu unamfungulia mlango wa kufanya sanaa ya keki.

Licha ya kuwa na CPA, Scolastica au Scola ana shahada ya biashara kwenye masuala ya fedha (Bachelor of Commerce in Corporate Finance), anazungumza na Nipashe wiki iliyopita jijini Dar es Salaam, akisema, ameanzisha kampuni ya Ola Delicious na sasa ni Mtendaji Mkuu –CEO.

Kwa wengi, sanaa ya keki inaweza kuonekana kuwa jambo gani, lakini binti huyu mhitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, anasema ndiyo maana ya ubunifu na ujasiriamali.

Akifanya shughuli zake Tegeta, anasema anatumia sanamu za keki kufanikisha ujasiriamali na kufikisha ujumbe na simulizi mbalimbali za maisha ikiwamo harakati za ukombozi wa mwanamke kimapinduzi au 'feminism'.

Anaeleza kuwa licha ya kusoma na kupata shahada ya juu CPA na 'Bachelor of Commerce in Corporate Finance' malengo yake ni kwenda mbali na kuwa mbunifu zaidi na kutumia 'sculpture' au sanamu za kuchonga na kuchangia kufanikisha ndoto za watu na waharakati ambazo hazikutimia.

Nipashe inakutana na Scola katika maonyesho ya Tamasha la Jinsia Tanzania linaloandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) yaliyomalizika Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, akieleza kuwa anatumia ubunifu na kazi yake hiyo kuonyesha kuwa wapo watu ambao wana ndoto lakini hawajaweza kuzitimiza na kuwahakikishia kuwa zinaweza kufanikiwa.

Analenga pia kuwagusa na kuwaenzi wanawake mashujaa walioleta mabadiliko kwenye jamii katika nafasi na nyakati mbalimbali.

Mathalani, amesoma uchumi na uhasibu lakini ana ndoto nyingine ya kuwa na kampuni na kuleta jambo jipya katika jamii la kutumia sanamu za keki kufundisha ujasiriamali na kufikisha ujumbe wa uhalisi wa changamoto, mafanikiko, ushujaa na mambo mengi watu wanayopitia.

Anaeleza kuwa kazi za kufikia ndoto zake zinafanikishwa na Mfuko wa Ruzuku (ufadhili) kwa Mashiriki Watetezi wa Haki za Wanawake (WFTT), na kwa uhisani wake amendaa kazi ya sanaa ya kike inayozungumzia ndoa ya utotoni ikipewa jina la 'Ndoto ya Kalista' iliyoumiza na kumtesa binti mmoja ambaye keki hiyo inaelezea kisa chake.

"Katika harakati za kutumia sanamu ya keki ninafikisha ujumbe na simulizi mbalimbali kuanzia mafunzo ya ujasiriamali kwa kinamama na mabinti pia zitaleta ujumbe kuhusu athari za ndoa za utotoni, ukatili dhidi ya wanawake na watoto na sambamba na harakati za kuwatetea na kuwawezesha."

Aidha, anasema Mfuko wa WFTT ndiyo unafadhili kazi yake katika tamasha hilo ambalo katika maonyesho ameonyesha sanamu ya keki ya ndoa ya utotoni iliyojaa maumivu, machozi na kukatishwa tamaa.

Scola anafafanua kuwa katika maonyesha anawasilisha ujumbe unaozungumzia ndoto ya binti aliyeolewa utotoni ambayo haikuwa na tija licha ya kwamba alitegemea kuwa ingekuwa ni jambo jema katika maisha yake.

Inabeba ujumbe wa binti ambaye alinyanyaswa kingono utotoni na jamaa wa karibu naye, lakini aliozwa utotoni jambo alilolifurahia akiamini kuwa lingempa amani na kuondoa mateso aliyopitia, lakini ndoa hiyo ya kufungwa kanisani ilikuwa ni shubiri kwake na mtoto aliyempata.

**NDOTO**

Scola analenga kujikita katika kuwekeza kwenye sanaa ya kuchonga, kufinyanga na uhandisi ukiwemo wa majengo na maumbo mbalimbali yanayoonyesha keki kwa nia ya kuendeleza ndoto yake inayotokana na ujasiriamali wa keki.

"Ndoto yangu, natarajia kuwa na kituo au 'senta' ya kufundisha sanaa ya keki kiujasiriamali na ubunifu zaidi lakini ikihusisha harakati za kutetea wanawake na watoto ili kupata haki na maendeleo na kufikia usawa kijinsia, fursa na haki sawa kwa wote ."

Anasema keki ni kitu kinachopendwa na kuliwa na wengi hivyo anatamani kukiendeleza kwenye maeneo mbalimbali kiubunifu kwa mfano mara nyingi kuna vifaa vya kutengeza keki vyenye maumbo ya duara, mraba au pembe lakini hakuna utaalamu wa kuchonga keki.

> Analenga pia kuwagusa na kuwaenzi wanawake mashujaa walioleta mabadiliko kwenye jamii katika nafasi na nyakati mbalimbali.

Msomi huyu wa uhasibu anaeleza kuwa keki inayoifikisha kwenye maonyesho hayo ni ya kuchonga, akimaanisha kuwa anakanda unga na kuanza kuuchonga kupata sanamu ya bibiharusi na kwamba hakuna kifaa kinachoweza kutengeneza umbo hilo.

Kadhalika Scola anatarajia kutumia mbinu za ufinyanzi kutengeneza keki na kufikisha ujumbe mbalimbali na pia kuleta burudani kwa walaji na wajasiriamali.

Pamoja na Scola wapo mabinti wanaojumuika naye kwenye maonyesho hayo wanaosimulia changamoto zao, wakisema katika umri mdogo wamepitia ukatili wa kijinsia hasa kunyanyaswa kingono na jamaa wa karibu nao.

Baadhi (majina tunayahifadhi), wanasimulia chuki wanazokutana nazo ndani ya familia zilizosababisha wazazi wao kutengana na maisha yao kusambaratika katika umri mdogo.

"Nilizaliwa kwenye familia nikiishi na baba na mama, lakini shemeji na wifi zake mama walikuwa hawampendi na kumzulia mambo mengi ambayo yalisababisha baba kumtelekeza mama na sisi watoto, akikimbia nyumba na familia." Anasema binti.

Anaongeza kuwa ugumu wa maisha ulimtoa shuleni alipokuwa akilipiwa na baba yake na kuhamishiwa kwenye shule ya umma. Lakini umaskini wa kipato ulisababisha afanye kazi za kupika keki na kuziuaza ili wapate hela ya kula na mwisho alifeli shuleni.

Anasimulia zaidi kuwa maisha yalikuwa magumu ndipo mama yake mzazi alipouza nyumba na kuhamia kwenye chumba cha kupanga ambako aliishi humu na watoto wake zaidi ya wawili.

Hata hivyo, maisha yalikuwa magumu zaidi akakosa kodi na kurudi nyumbani kwa bibi mzaa mama yake ambako nako ilikuwa ni matatizo, vyote vikisababisha watoto hao kusoma na kukosa haki nyingine za msingi.

Mabinti hao wanataka kuwe na ushirikiano mkubwa baina ya familia, asasi za kirai, jamii na serikali ili kuripoti na kukabiliana na matukio ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto ambayo zama hizi yameongezeka.




Scolastica Sultan, akitoa maelezo kuhusu ujumbe ulioko kwenye sanamu ya keki iliyopewa jina la 'Ndoto ya Kalista'. **PICHA: MWANDISHI WETU**



## NEC yapongezwa kwa kuleta vifaa vya kutunza taarifa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

BARAZA Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Wilaya ya Dodoma limepongeza hatua ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa kuleta vifaa vipya vitakavyotumika kwa ajili ya kutunza taarifa za wapigakura.

Hivi karibuni Mkurugenzi wa (NEC), Ramadhan Kailima akizungumza na waandishi wa habari alisema kuwa wanatarajia kufanya uboreshaji wa majaribio wa daftari la kuduma la wapiga kura kwa kutumia vifaa hivyo kwa ajili ya uboreshaji wa daftari la wapigakura.

Mwenyekiti wa BAKWATA Wilaya ya Dodoma, Omary Bashiru, akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu NEC kuleta vifaa hivyo alisema kutokana na uboreshaji huo wa vifaa Watanzania wanatarajia kuona uchaguzi ujao ikiwamo wa serikali za mitaa na ule wa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 unafanyika kwa haki kwa vyama vyote vitakavyojitokeza.

Alisema kuwa ni matarajio ya Watanzania kupitia vifaa hivyo vya kisasa vyama vya siasa vitakavyojitokeza wagombea wao kugombea waamini kuwa kutatendeka haki kwa kutunza taarifa mbalimbali zinazohusu wapigakura wao.

Aidha, BAKWATA iliwaomba wapigakura kutoka vyama vyote vya siasa kutokufanya makosa kwenye kuchagua viongozi wao bali wachague watakaoisaidia nchi kuleta maendeleo bila kuangalia chama wanachowakilisha.

Pia aliwaomba wananchi watakaojitokeza kugombea kwenye uchaguzi hizo wajitafakari kwanza, badala ya kukurupuka kwa kufuata ushabiki wa vyama vyao husika.

Alisema Watanzania wanahitaji viongozi watakaosaidia nchi katika kuleta uchumi na kuhamasisha maendeleo katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, afya, elimu, ufugaji na uvuvi bila kujali itikadi yoyote.

**Alisema kuwa ni matarajio ya Watanzania kupitia vifaa hivyo vya kisasa vyama vya siasa vitakavyojitokeza wagombea wao kugombea waamini kuwa kutatendeka haki kwa kutunza taarifa mbalimbali zinazohusu wapigakura wao.**

# Wanaofanya biashara maeneo yasiyo rasmi wapewa salamu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Jiji la Dodoma, John Kayombo, amesema operesheni ya kuwaondoa machinga waliojenga vibanda vya biashara katika maeneo yasiyo rasmi ikiwamo pembezoni mwa barabara itaendelea kama kawaida.

Alitoa maelezo hayo juzi wakati akijibu hoja katika kikao cha baraza la madiwani cha robo mwaka.

Madiwani hao walitaka kujua mkakati uliopo wa Jiji la Dodoma kuwaondoa wafanyabiashara wadogo (machinga) ambao wameanza kurudi mitaani kufanya biashara na wengine kujenga vibanda kwenye maeneo ya majengo ya taasisi na wale wanaopanga katika barabara zinazotumiwa na watembea kwa miguu. Kayombo, alisema kuwa mkakati wa Jiji la Dodoma ni kuhakikisha hakuna wafanyabiashara wadogo watakaoruhusiwa kufanya biashara zao kwenye maeneo ambayo hayaruhusiwi na kama wameanza kurudi wataondolewa.

"Niwahakikishie madiwani wa Jiji la Dodoma kuwa hakuna kibanda chochote kilichopo kwenye maeneo ya taasisi za kiserikali, nyumba za watu binafsi kwenye barabara za waenda kwa miguu watakaoachwa, lazima watabomolewa," alisema.

Aidha, alisema kila kata kuna masoko yake hivyo haoni sababu ya wafanyabiashara wadogo kurudi mitaani na kujipangia kufanya biashara maeneo ambayo hayaruhusiwi.

Awali wakichangia kwenye kikao hicho, Diwani wa Kata ya Kikuyu Kusini, Anselem Kutika, alisema machinga tayari wameanza kuzagaa mitaani na kupanga biashara maeneo yaliyozuiliwa kufanya hivyo.

Kutika, alisema Jiji la Dodoma linatakiwa kufanya maamuzi yake ambayo hayatajirudia kama hili la wafanyabiashara wadogo hao kuanza kurudi kwenye maeneo waliyoondolewa baada ya kutengewa sehemu zingine ikiwamo masoko yaliyopo katika kata zao.

Naye Diwani wa Viti Maalumu, Joyce George, aliwaomba madiwani kushirikiana na Jiji la Dodoma kutoa elimu kwa wafanyabiashara hao ili kuwaepusha na hasara wanazozipata za kubomolewa na kunyang'anywa bidhaa zao pale wanapokutwa kwenye maeneo yasiyoruhusiwa.




Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha za Kigeni wa Benki ya Absa Tanzania, Esther Maruma (wa pili kulia) na Kaimu Mkurugenzi wa SOS Childrens Villages, Dorothy Ndege, wakitia saini kuashiria makabidhiano ya msaada wa fedha Sh. milioni 10 kutoka benki hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Ikiwa ni mwendelezo wa benki hiyo kurudisha faida wanayoipata kwa jamii. Wanaoshuhudia kutoka kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Wateja Wakubwa wa Absa, Nellyana Mmanyi na Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano, Aron Luhanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shirika lakarabati na kufufua visima 38 Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Empower Society Transform Lives (ESTL) kwa ufadhili wa Taasisi ya MO Dewji Foundation limefanikiwa kukarabati na kuvifufua visima 38.

Visima hivyo ni vile ambavyo baadhi vilikuwa havitoi maji katika kata 12 za Manispaa ya Singida kwa lengo la kuwawezesha wananchi kupata huduma ya majisafi na salama.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa shirika hilo, Joshua Ntandu alisema juzi kuwa baada ukarabati na ufufuaji huo kukamilika umewezesha zaidi ya wananchi 38,400 kuondokana na tatizo la uhaba wa maji katika maeneo yao.

Ntandu alisema kabla ya ufufuaji na ukarabati huo kufanyika, shirika hilo lilifanya upembuzi yakinifu na kugundua kuna visima 45 vya maji vilivyochimbwa wakati Mohammed Dewji akiwa Mbunge wa Singida Mjini miaka kadhaa iliyopita lakini vilikuwa havifanyi kazi tena kutokana na hitilafu mbalimbali.

Alisema: "Katika shughuli zetu za kila siku, ikiwa ni pamoja na mapambano dhidi ya ukeketaji, tuliona suala la afya na usafi kwa wananchi ni suala muhimu na katika kufuatilia suala hilo tulibaini kati ya visima 45 ni visima 38 pekee vinavyoweza kufufuliwa na kukarabatiwa vianze kutoa huduma ya maji kwa wananchi".

Alisema mpango wa ufufuaji wa visima hivyo ulikuwa ni wa muda mfupi na kwamba mkakati uliopo shirika hilo wamekubaliana na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA) kuunganisha maji yanayotolewa na mamlaka hiyo kwenye kata ambazo zipo pembezoni mwa mji.

Ntandu alisema mpango huo utasaidia kuongeza mtandao wa upatikanaji wa maji katika Manispaa ya Singida kutoka asilimia 86.4 hadi kufikia asilimia 96.4 ifikapo mwaka 2026 na kwamba maji ya visima vyote vilivyofufuliwa na kukarabatiwa yalipimwa katika maabara na kubainika yanafaa kwa asilimia 93 kwa matumizi ya wananchi.

Aliongeza kuwa mpango mwingine uliopo ni kwa ESTL na Mo Dewji Foundation kufanya ushirikiano na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Singida ili kupanua wigo wa upatikana wa maji katika wilaya, kata na vijiji vyote vilivyopo katika mkoa huo.

Aidha, Ntandu alihimiza umuhimu wa kuvitunza visima hivyo ili viweze kudumu kwa muda mrefu na kutengeneza mpango mzuri utakaotumika kuvifanyia matengenezo vitakapokuwa na changamoto ya kuharibika kwa kuwa wao hawatahusika na matengenezo hayo.

Mhandisi wa maji wa shirika hilo, Edward Barnaba, alisema visima vimekuwa vikiharibika kutokana na kuingia kwa mchanga na watoto kuweka mawe kwenye pampu ya kusukuma maji na kuharibu mfumo. Hivyo alishauri maeneo vilipochimbwa iachwe nafasi ya mita 60 na kuzungushiwa uzio ili mazingira yake yasiharibiwe tena.

Fundi Sanifu Mkuu Ubora wa Maji, Maabara ya Singida, Shifaya Munisi, alisema baada ya kupima ubora wa maji na kufufuliwa kwa visima hivyo yameonekana kuwa ni safi na salama kwa matumizi ya binadamu.

Mwakilishi wa Mo Dewji Foundation katika ufufuaji wa visima hivyo, Janeth Mashauri, aliwataka wananchi ambao visima vyao vimefufuliwa wavitunze kwani ni mali yao.



# Waiomba serikali kuharakisha ujenzi wa Daraja la Lualaje

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKAZI wa vijiji vya Lualaje na Mwiji vilivyopo Kata ya Lualaje Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya wameiomba serikali kuharakisha ujenzi wa Daraja la Lualaje ili liwasaidie kurahisisha mawasiliano kati ya vijiji hivyo na maeneo mengine ya wilaya hiyo.

Aidha, wamesema daraja hilo linatakiwa lijengwe kabla ya mvua kuanza kunyesha wakidai kuwa hali itakuwa mbaya zaidi na watashindwa kusafirisha pembejeo kwenda mashambani na pamoja na kusafirisha mazao.

Walitoa ombi hilo wakati wa ziara ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera ambaye alifanya ziara kwenye eneo hilo kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo pamoja na kusikiliza kero za wananchi.

Mmoja wa wananchi hao, Yusuph Mwangoka aliishukuru serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo ambalo pia linaunganisha kata yao na kata jirani ya Mapogoro.

Alisema wananchi wa maeneo hayo wamejikita katika shughuli za kilimo na kwamba hivi sasa wanatumia gharama kubwa kusafiri pamoja na kusafirisha mazao yao.

Alisema daraja hilo likikamilika litawapunguzia gharama za maisha na adha ya usafiri wanayoipata sasa ambapo walisema mvua ikianza kunyesha kabla daraja hilo halijajengwa hakutakuwa na gari yoyote itakayokwenda.

Mwangoka alisema wananchi wa kata hizo wanalima zaidi tumbaku ambapo mtumba mmoja wa tumbaku wanasafirisha kwa Sh.5,000 kutoka shambani kwenda kwenye maghala ambayo yapo upande wa pili na kwamba daraja hilo likikamilika gharama zitapungua hadi kufikia Sh. 1400.

"Hili daraja ni kiungo muhimu sana kwetu kwa sababu ndilo tunalitegemea kusafirisha mazao yetu, mvua ikianza kunyesha tutabaki kisiwani huku, kwahiyo tunakushukuru sana Mkuu wa Mkoa kwa kututembelea maana tunaamini utatusaidia kuongeza msukumo," alisema Mwangoka.

Awali akisoma taarifa ya ujenzi wa daraja hilo, Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Wilaya ya Chunya, Mhandisi Emmanuel Kayola, alisema mradi huo unagharimu Sh. milioni 200 na kwamba mpaka sasa ujenzi umefikia asilimia 75.

Alisema mpaka sasa mkandarasi anaendelea na ujenzi na kwamba wanatarajia atakamilisha katikati ya Desemba mwaka huu na kuanza kutumika na hivyo akaahidi wakala huo kuendelea kusimamia na kufuatilia hatua zote za ujenzi ili wananchi wanufaike na daraja hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alimtaka mkandarasi kufanya haraka ujenzi wa daraja hilo ambalo alidai ni tumaini kwa wasafirishaji wa mazao na wanafunzi wanaotegemea kuvuka wanapokwenda shuleni.

Pia aliwataka uongozi wa vijiji na kata hizo kushirikiana na mkandarasi katika ulinzi wa vifaa vya mradi ili visiibiwe kwa maelezo kuwa yapo baadhi ya maeneo umejitokeza wizi wa vifaa vya ujenzi wa miradi ya maendeleo hali inayorudisha nyuma juhudi za serikali za kuwaletea maendeleo wananchi.



Mmoja wa wafugaji wanaodaiwa kuvamia msitu wa hifadhi wa nyuki Kipembawe uliopo katika Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, akiendelea kuswaga ng'ombe wake kwenda machungani mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakulima wa mahindi wilayani Njombe wapewa milioni 583/-

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

CHAMA cha Msingi cha Ushirika wa Wakulima wa Mahindi (Ibumila AMCOS) kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, kimepokea Sh. milioni 583 kutoka kwa wadau wa maendeleo kwa ajili ya kukuza zao hilo.

Akizungumza na wanachama hao wakati wa kukabidhi hundi ya mfano, Mratibu wa shirika lisilo la kiserikali la USADF, Girriad Nkini, alisema shirika hilo limeamua kuingia mkataba na wakulima hao ili kuwasaidia kuboresha kilimo cha mahindi kuwa cha kisasa.

Alisema pamoja na kiasi hicho cha fedha watafanya jitihada za kuhakikisha wanawatafutia masoko ya uhakika ili kuongeza thamani ya zao hilo.

"Pia tutawaongezea usafiri wa pikipiki na gari la kuwasaidia kuchukua mahindi na kusambaza ule unga madukani na maeneo mengine," alisema Nkini.

Meneja Mradi kutoka USADF nchini, Irene Mwakisese, alisema wameamua kuingia mkataba na chama hicho cha ushirika ili kuongeza uzalishaji wa zao la mahindi wilayani Njombe.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Christopher Sanga, alipongeza shirika hilo kwa kutoa fedha hizo ambazo zitasaidia kuongeza thamani ya zao la mahindi mkoani Njombe.

Mmoja wa wakulima wa chama hicho, John Nyagawa alisema kwa muda mrefu wamepata changamoto ya kukosa soko la uhakika la mahindi, hivyo wanaamini mradi huo utakuwa mkombozi.

# Wananchi watakiwa kulipa malimbikizo ankara za maji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (MBEYA-WSSA) imewataka watumiaji wa huduma ya maji kulipa ankra zao kwa wakati ili mamlaka hiyo iweze kujiendesha na kutoa huduma bora kwa wananchi mkoani humo.

Mkurugenzi wa Mbeya-WSSA, Gilbert Kayange, alitoa wito huo wakati akizungumza na wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi kwenye mkutano ulioandaliwa na mamlaka hiyo kwa lengo la kusikiliza kero za watumiaji wa huduma ya maji.

Kayange alisema serikali inatumia gharama kubwa kwenye utekelezaji wa miradi ya maji na hivyo wananchi wanapaswa kutambua kuwa ankra wanazolipia wanachangia sehemu ya gharama hizo na kwamba gharama kubwa inabebwa na serikali.

"Serikali inatoa gharama kubwa kujenga miradi ya maji, watumiaji mnapaswa kutimiza wajibu wenu wa kulipia ankra ili kuendelea kuendesha miradi hiyo, tunajitahidi kadri tuwezavyo kuhakikisha mnapata huduma," alisema Kayange.

Vilevile alisema wananchi wanapaswa kutambua thamani ya maji safi wanayopata kabla hawajalalamikia huduma wanazopata ikiwamo ankra wanazolipia.

Wakizungumza katika mkutano huo wananchi hao waliomba mamlaka hiyo kuingia kwenye mfumo wa kisasa wa lipa kabla kwa wananchi wake ili watumiaji walipe kulingana na matumizi yao.

Mmoja wa wananchi hao, Joseph Sote, alisema huduma ya maji imekuwa ikikatika mara kwa mara na hivyo kusababisha wananchi kukosa huduma lakini bado wanatakiwa kulipa ankra.

Hata hivyo Kayange alisema tayari wameanza kutoa mita za luku za maji kwa kwa kampuni kubwa, lakini wakabaini kuwa mfumo huo una tatizo kwa maelezo kuwa unatumia teknolojia ya kisasa ambayo uendeshaji wake ni gharama.

Alisema wanaendelea kuboresha mfumo huo ili waanze kusambaza kwa wananchi wengine.

Katika hatua nyingine Kayange alimwagiza Mkurugenzi wa Maji Mbalizi kuwachukulia hatua baadhi ya watumishi wanaowazuia wananchi kufikisha kero zao kwa viongozi wa mamlaka hiyo kwa maelezo kuwa wananchi wanayo haki ya kueleza kero zao pale wanapoona upungufu kwenye utoaji wa huduma ya maji.

**"Serikali inatoa gharama kubwa kujenga miradi ya maji, watumiaji mnapaswa kutimiza wajibu wenu wa kulipia ankra ili kuendelea kuendesha miradi hiyo, tunajitahidi kadri tuwezavyo kuhakikisha mnapata huduma," alisema Kayange.**



## ACT-Wazalendo yataja athari kupanda bei za mafuta

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kupanda kwa bei za mafuta visiwani Zanzibar siyo jambo la kawaida na linazidi kuathiri wananchi wa visiwa hivyo hasa wenye kipato cha chini.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari juzi, Katibu wa Habari, Uenezi, Mawasiliano na Umma wa chama hicho, Salum Bimani alisema miongoni mwa athari hizo ni mfumko wa bei wa bidhaa mbalimbali.

Alisema wafanyabiashara hufidia gharama hizo za usafiri kwa kupandisha bei bidhaa zao.

Alisema athari zingine ni wafanyabiashara wadogo kufunga biashara zao kutokana na kupanda kwa gharama za uendeshaji ambapo kupanda kwa gharama za mafuta kunasababisha kufa kwa biashara zao.

Pia, alisema athari hizo kutasababisha kuongeza mzigo mkubwa wa maisha kwa wananchi wa kawaida ambaye atakuwa anapambana na kuzimudu gharama hizo za kununua bidhaa kama vile vyakula vinavyozalishwa ndani na nje ya Zanzibar.

Bimani alisema ACT inaitaka serikali kufanya mapitio ya mfumo uliopo wa uingizaji mafuta ya jumla ambao una ukiritimba wa muda mrefu na mfumo huo unapunguza ushindani.

"ACT Wazalendo tunaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuangalia upya mfumo wa kodi za serikali katika sekta ya nishati na mafuta nchini ili kuweka unafuu kwa wananchi. Kwa mfano, katika miaka ya nyuma kulikuwa na sera maalum ya kudhibiti bei ya mafuta ya taa kwa kuyaondolea kodi zote inapobidi" alisema Bimani.

Hata hivyo, aliitaka serikali kutazama upya gharama za uingizaji wa mafuta kutoka katika Bandari ya Dar es Salaam kuja Bandari ya Zanzibar, kuna uwezekano mkubwa kuwapunguzia wananchi mzigo huo mkubwa ambao wanaubeba.

Alisema matangi ya mafuta ya Serikali ya Mtoni ambayo sasa yamekodishwa yalijengwa kwa madhumuni hayo, hivyo ni wakati kutafakari upya umuhimu wa jambo hilo.

Alisema kwa kipindi cha miezi mitano bei ya mafuta ya petroli kwa mujibu wa Mamalaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) bei imepanda kutoka Shilingi 2,700 kwa Julai mpaka Shilingi 3,187 Novemba, ongezeko la shilingi 487 sawa na wastani wa asilimia 15.2.

Alisema kwa bei ya mafuta ya dizeli yamepanda kutoka shilingi 2,746 kwa Julai mpaka shilingi 3,323 Novemba, ongezeko la shilingi 577 sawa na wastani wa ongezeko la asilimia 17.36.

# Waziri ataja chanzo kunyesha mvua kubwa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema athari za mvua zinazoendelea ni matokeo yanayosababishwa na binadamu kuharibu mazingira ikiwemo kukata miti.

Aliyasema hayo juzi wakati akizindua Taasisi ya Maendeleo Zanzibar (Tamaza) uliofanyika viwanja vya Kisonge Mjini Zanzibar, ambapo miongoni mwa malengo ya taasisi ni kudumisha mazingira.

Alisema majanga yanayotokana na athari hizo za mvua, yanayotokana na uharibifu wa mazingira, miti inatoa hewa ya Oxygen ambayo inahitajika kwa afya kwa kusaidia binadamu na viumbe hai kuweza kuishi.



"Kuna ujenzi wa kasi kubwa ya ujenzi mbalimbali lakini tunapokata miti hatupandi miti hali ambayo inasababisha athari za majanga mbalimbali ya kimazingira" alisema.

Alisema serikali kupitia wizara yake ifikapo mwaka 2025 inatakiwa kuhakikisha imeotesha miti isiyopungua milioni mbili ili kujenga Zanzibar ya kijani na ya watu wenye afya.

Alisema ikitokea mabadiliko ya tabianchi katika maeneo yoyote duniani, kuna sehemu jitihada za utunzaji wa mazingira zimepungua na kwa Zanzibar kwa sasa inatarajia kuvuna hewaukaa na haiwezi kupatikana endapo kutakuwa na uchafuzi wa mazingira.

Shamata alisema serikali ina mpango wa kuonesha utayari wa kutaka mabadiliko chanya yenye kuonekana kwa kila mtu kwa kupanda miti katika mikoa mitano, ili kurejesha uhalisia wake na kwa mwaka huu wanakusudia kupanda miti milioni moja.

Alisema miti itapandwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Tamaza ambapo miti 400,000 itapandwa kisiwani Pemba na 600,000 Unguja ikiwa na lengo ya kuifanya Zanzibar ya kijani.

Naye Mkuu wa Mkoa Mjini Magharib, Idrissa Kitwana Mustafa alisema kuwa watahakikisha mji huo unakuwa wa kijani ili kuweka mandhari nzuri kwa sababu mji huo ndio kimbilio la watu wengi.

Katibu wa Tamaza, Iddi Thabit alisema taasisi hiyo imelenga kupanda miti katika miradi ya ujenzi iliyojengwa na serikali ili kutunza mazingira na kuilea miti hiyo.

Alisema wanafanya hivyo kuunga mkono juhudi za serikali zinazofanywa kuirejesha Zanzibar ya kijani na ndio maana wakaanzisha kampeni hiyo.



Mpita njia akipita kwenye uzio ili kuvuka upande wa pili wa Barabara ya Morogoro eneo la Mbezi Mwisho Dar es Salaam juzi, badala ya kupita juu ya daraja la waenda kwa miguu, kitendo ambacho kinaweza kuhatarisha maisha yake kwa kugongwa na magari. **PICHA: SABATO KASIKA**

## ZUPSCA yaleta mchango chanya sekta ya afya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Afya Zanzibar, Hassan Khamis Hafidh, amesema kuwepo kwa Chuo Kikuu cha Zanzibar (ZUPCSA) kumefanikisha kuanzisha fani mbalimbali ikiwemo saikolojia ambayo imeleta mabadiliko katika sekta ya afya.

Alisema hayo jana wakati akifungua Jukwaa la Siku ya Saikolojia lililoandaliwa na ZUPCSA lenye kauli mbiu isemayo 'afya ya akili na tiba ya saikolojia ni haki kuu ya kibinaadamu'.

Alisema suala la utoaji wa huduma za afya unahitaji utafiti hivyo kuwepo kwa fani hiyo kutachangia huduma bora za kiakili.

Pia, alitumia nafasi hiyo kuwataka wataalam wa fani ya saikolojia kutumia lugha nzuri kwa wagonjwa ili kuongeza imani kwa jamii juu ya utoaji wa huduma ya afya nchi.

Aidha, aliwataka vijana kuendelea kulinda amani na utulivu uliopo nchini ikiwa ni sehemu ya kuendelea taifa lenye kuchangia maendeleo.

Vilevile, aliupongeza uongozi wa ZUPCSA kuanzisha fani ya saikolojia ambayo ni muhimu kwa maslahi ya taifa.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdalla Saidi aliwataka wanasaikolojia kufanya utafiti wa chanzo cha kujitokeza matukio ya udhalilishaji nchini ili kupata matokeo yatakayopunguza vitendo hivyo.

Aidha, aliwataka watendaji wa fani hiyo kufanya kazi kwa bidii hasa utoaji wa huduma kwa jamii ili kuongeza ufanisi.

Naibu Makamu Mkuu wa ZUPCSA, Dk.Rashid Juma Rashid alisema chuo kinafanya kazi kubwa ya kufundisha wataalam wa saikolojia na vijana waliiosomea fani hiyo wanatoa mchango mkubwa katika jamii.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(CAP. 117)**
**DEED POLL ON CHANGE OF NAME**

BY THIS DEED I, the undersigned SHAMIRA NASORO DULELE of P.O.BOX 166, MOROGORO, do hereby absolute renounce, relinquish and abandon the use of my former name of MWAJINA NASSORO UDULELE which was wrongly written in my Identification Card (NIDA) Number 19470701-67220-00003-10 and SHAMILA N. DULELE which was wrongly written in my ID of KADI YA MPIGA KURA number T-1000-6813-923-0 in lieu thereof I assume and adopt the name of SHAMIRA NASORO DULELE in my National Health Insurance Fund.


AND IN PURSUANCE of such change of name as aforesaid I HEREBY DECLARE THAT I shall at all-time hereinafter in all Records, Deeds and instruments, in writing in all action and proceedings and in all dealings and transaction and upon all accessions Whatsoever use and sign the said name of SHAMIRA NASORO DULELE as my name in lieu of the said MWAJINA NASSORO UDULELE and SHAMILA N. DULELE so renounced as aforesaid.

AND

I HEREBY AUTHORISED AND REQUEST, all persons to designate, describe and address me by such adopted name of SHAMIRA NASORO DULELE.

I, SHAMIRA NASORO DULELE make this declaration conscientiously believing the same to be true and in accordance with the provisions of the Oath (Judicial Proceedings and Statutory Act, as Revised Edition 2019)

IN WITNESS WHEREOF, I have unto subscribed my adopted and substituted name of SHAMIRA NASORO DULELE on the day and in the manner hereinafter appearing.




## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**BARAKA SAMWEL MANYANDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 652 DFD.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya Polisi:
**PHQ/ARU/ARU/6806/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JULIUS MARAKI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 827 DCQ aina ya KINGLION. Chassis namba LGVSKP805MZ811077. Engina namba NOSK162FMJ2100375437.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi:
**PHQ/ARU/ARU/6100/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**CHARLES CLEMENCE MALLYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya **BAJAJI** yenye namba za usajili **MC 155 CEM** aina ya **TVS ,** Chassis **No.MD6M14PA3K4AA0291.** Ye yote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**PHQ/DOD/DOD/8434/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi (V)**
**Kituo cha Arusha Chini Mkoa ................**
**Shauri la Ndoa 20, 2023.**
**Jina la Mdai Salima Brian Mushi.**
**Jina la Mdaiwa Amani Rashid Mallya.**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa:**
**AMANI RASHID MALLYA MKAZI WA MOSHI 0722 034 446,**
Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yao kwamba (eleza hapa habari za Madai)
**MADAI YA TALAKA, MGAWANYO WA MALI ULEZI WA WATOTO MATUNZO YA WATOTO.**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 20 mwezi 11 mwaka 2023 saa 03:00 asubuhi kwa mujibu wa maombi hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,
Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 03 mwezi 11 Mwaka 2023

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
ARUSHA CHINI

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NAMBA 144 YA MWAKA 2023**
**SAID MZAMIL NASSOR............ MRUFANI**
**DHIDI YA**
**HEMED ALLY MUBA..........1. MJIBU RUFANI**
**YAKUB ABDULRAHNAN MNETE.........2. MJIBU RUFANI**

**KWA: HEMED ALLY MUBA,**
**DAR ES SALAAM.**

**YAKUB ABDUL-RAHNAN,**
**DAR ES SALAAM.**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mrufani aliyetajwa hapo juu amefungua shauri la maombi ya rufaa ya madai dhidi yenu, maombi ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi hayo zinazopatikana katika mahakama hii, hivyo basi, mnatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii, wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wenu ambaye anaruhusiwa kisheria siku ya tarehe **05/12/2023** saa tatu (3:00) asubuhi mbele ya mhe. E.E. KAKOLAKI, kujibu madai hayo dhidi yenu. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.

**ANGALIA:**
Kama msipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikathibitisha kuwa mmepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wenu.

HATI hii imetolewa kwa MKONO wangu na CHAPA ya mahakama leo hii tarehe 02 mwezi 11/2023

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU
KANDA YA DAR ES SALAAM

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**





TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Hospitali zafungwa rasmi Gaza

## • UNDP: Wanafunzi 625,000 hawaendi shule



Wanajeshi wa Israel, wakimfariji mama wa mwanajeshi mwenzao Sergey Shmerkin, aliyeuawa Kaskazini mwa Gaza, kwenye maziko eneo la Kiryat Shmona, Israel jana. **PICHA: BBC**

**Na Christina Mwakangale**

ZINATIMIA siku 38 tangu Jeshi la Israel lilipoanza mashambulizi katika Ukanda wa Gaza, kutokana na kundi la Hamas, kushambulia kusini mwa Israel na kusababisha vifo 1,400.

Wakati siku hizo zikitimia na kutokuwapo mafanikio ya kidiplomasia na juhudi za Umoja wa Mataifa (UN), kwamba vita hivyo visitishwe, hakuna matumaini hayo. Mara kadhaa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amenukuliwa akisema jeshi lake halitorudi nyuma.

Zipo athari kadhaa zilizojitokeza kwa kipindi hicho cha mwezi mmoja na wiki moja, ikiwamo za kiuchumi kwenye eneo la Ukanda wa Gaza.

Aidha, vifo vya Wapalestina vinaarifiwa na Wizara ya Afya Gaza kwamba vinazidi 11,000 kati yake 4,000 ni watoto. UN, jana, ilipeperusha bendera nusu mlingoti katika maeneo yake duniani, kuwakumbuka wenzao 101 waliopoteza maisha huko Gaza.

Kadhalika, Wizara ya Ulinzi ya Israel (IDF), limesema limepoteza wanajeshi wasiopungua 44 waliouawa katika vita huko Gaza.

### HOSPITALI ZAFUNGWA

Hospitali kubwa zaidi zilizotegemewa na Gaza, Al-Shifa na kituo kingine kikubwa, Al Quds, vilitangaza kuwa zinasitisha shughuli zao zao rasmi.

Hospitali kaskazini mwa eneo la Palestina zimezuiwa na vikosi vya Israel na haziwezi kuwatibu wagonjwa, wafanyakazi wa matibabu wamesema.

> **UN, umeonya kwamba kiwango cha umaskini kinaweza kuongezeka zaidi, na kwamba ukanda huo, ni miongoni mwa maeneo yaliyo na kiwango cha juu cha ukosefu wa ajira duniani.**

Israel imesema inakabiliana na wapiganaji wa Hamas katika eneo hilo na kwamba hospitali zinapaswa kuhamishwa.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu akizungumza na shirika la televisheni ya Marekani CNN, amedai kwamba wapiganaji wa Hamas wanawazuia wagonjwa na watu kuondoka kutoka hospitalini.

Maofisa wa Wizara ya Afya Gaza, wanasema mazingira hayaruhusu wagonjwa kuhamishwa na hawajui watawapeleka wapi, wakati mashambulizi yanafanyika sehemu zote za Gaza.

Imesema kwamba hakuna Mpalestina atakaye kuwa na imani kuhusu kuhamishwa wagonjwa na watu wanaowashambulia.

Wafanyakazi wanasema mashambulizi ya Israel na ukosefu wa mafuta na dawa, ni hatari na vinaweza kusababisha vifo vya watu ambao tayari wanatibiwa katika hospitali hizo.

Rais wa Israel, Isaac Herzog amekanusha kuwa, Israel inashambulia hospitali kubwa zaidi huko Gaza.

Herzog, kwenye nakala iliyotafsiriwa kwa Kiarabu ilipatikana anasema: "Siku chache tu zilizopita katika chumba cha watoto ambacho kimegeuzwa kuwa kituo cha operesheni ya kijeshi cha Hamas."

Mkurugenzi wa hospitali, Mohammad Abu Salmiya, amesema kwamba kumekuwapo na mapigano katika maeneo yanayozunguka hospitali na kusababisha hofu kubwa miongoni mwa wagonjwa na maelfu ya watu walioko hupo kupata hifadhi.

Waziri Mkuu wa Israel, Netanyahu, amesema kwamba huwenda makubaliano yako karibu kufikiwa ya kuachiliwa huru kwa mateka takriban 200, ingawa hakutoa maelezo zaidi akihofia kuharibu mikakati.

Hata hivyo ofisa mmoja wa Palestina huko Gaza amemlaumu Netanyahu, kwa kuchelewesha na kuweka vizuizi, ili kufikia makubaliano ya awali ya kuachiliwa kwa mateka hao.

Aidha, Hilali Nyekundu ya Palestina, ilieleza kwamba vifaru vya jeshi la Israel vilikuwa mita 20 kutoka hospitali ya Al-Quds mjini Gaza na kuzusha hofu miongoni mwa watu 14,000 waloojificha eneo la hospitali tangu kuanza mapigano.

Madaktari wa Al-Shifa wanasema wanahofia kwamba watoto 36 waliosalia wanaohitaji matibabu ya uangalizi mkubwa wanaweza kufa huku shirika la misaada la Medical Aid kwa Wapalestina, likisema bila ambulensi, vifaa muhimu au hospitali ya kuwahamisha watoto wanaozaliwa kabla ya wakati, hakuna dalili inaweza kufanyika kwa usalama.

Israel imesema, Hamas ina kambi chini ya jengo la hospitali, madai ambayo yamekanushwa na Hamas.

Daktari wa Upasuaji, Marwan Abu Saada, anasema kwamba hospitali imekosa maji, chakula na umeme.

Akisema sauti za risasi na mabomu zilisikika hospitalini katika kila sekunde.

### ATHARI KIUCHUMI

Wakati vita ikiendelea, tayari athari zimeanza kubainika. Asilimia 63 ya wakazi wa Ukanda wa Gaza walikuwa wanaishi chini ya mstari wa umaskini kulingana na takwimu za Serikali ya Gaza kabla vya mgogoro huo, huku watu 390,000 wakipoteza kazi, tangu Oktoba 7, mwaka huu.

UN, umeonya kwamba kiwango cha umaskini kinaweza kuongezeka zaidi, na kwamba ukanda huo, ni miongoni mwa maeneo yaliyo na kiwango cha juu cha ukosefu wa ajira duniani.

Profesa Sultan Burakat, miongoni mwa waliohojiwa na televisheni ya Al Jazeera, kipindi maalumu kuhusu Gaza na hali ya uchumi tangu kuanza kwa vita anasema, ipo haja ya wakazi wa Gaza kufidiwa, ili kurejea kwenye hali yao ya awali

Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP), linasema uchumi wa eneo hilo utashuka kwa asilimia 12 mwaka huu na mwakani utashuka zaidi hadi asilimia tisa, huku likibaini asilimia 45 ya makazi ya watu yameharibiwa.

Ofisi ya Takwimu ya Palestina, inasema asilimia 63 ya vijana walikuwa hawana ajira na sasa wengi wao wanaishi kutokana na msaada wa kiutu, huko Gaza.

Kwa mujibu wa UNDP, hospitali 35 hazitoi huduma za kiafya pamoja na shule 40 zimeharibiwa na wanafunzi takribani 625,000 hawawezi kuendelea na masomo.

Wizara ya Afya Gaza, inasema makazi 212,000 yameharibiwa miongoni mwa hayo 35,000 yakiharibiwa kabisa.

***IMEANDALIWA KWA MSAADA VYANZO VYA HABARI KIMATAIFA***

## HABARI MICHEZO

# SHIME KUIANDAA TANZANITE KWENDA KUIMALIZA NIGERIA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 20 (Tanzanite), Bakari Shime, amesema ana matumaini makubwa na vijana wake kwenda kufanya vizuri katika mchezo wa marudiano wa kuwania kufuzu Kombe la Dunia kwa umri huo dhidi ya Nigeria.

Tanzanite Queens walilazimishwa sare ya bao 1-1 na Nigeria kwenye Uwanja wa Azam Complex, mchezo wa raundi ya tatu wa kutafuta nafasi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia kwa Wanawake U-20, zitakazofanyika mwakani nchini Colombia.

Akizungumza na Nipashe juzi baada ya kukamilika kwa dakika 90 za mechi hiyo, Shime alisema walicheza nyumbani, hivyo walitarajia kupata matokeo mazuri na haikuwa mipango yao kutoka na sare ya bao 1-1.

**Alisema walicheza kwa tahadhari kubwa na kuwaheshimu Nigeria kutokana na historia nzuri waliyo nayo dhidi ya Tanzania na kwamba amefurahishwa na kiwango kilichooneshwa na wachezaji wake.**

Shime alisema bahati mbaya hatukupata kile walichokitarajia vijana, walicheza vizuri kwa kufuata maelekezo kwa kujilinda na kushambulia, lakini walifanya makosa na kuadhibiwa.

"Tulicheza kwa kuwaheshimu sana Nigeria kwa sababu ya historia nzuri waliyo nayo kwetu, kwani mara ya mwisho kucheza nao kwenye mashindano haya walitufunga mabao sita.

"Sare na Nigeria kwetu siyo mbaya na mechi hii haijaisha, naamini vijana wataenda kufanya vema ugenini kwa sababu wameshamjua vema mpinzani wetu," alisema Shime.

Aliongeza kuwa mchezo huo uko wazi na matarajio yao makubwa ni kwenda ugenini kupata matokeo mazuri katika mechi hiyo ya marudiano.





Edson Julius (kulia), akimtoka mchezaji mwenzake, Juvenali Erzandar, wakati wakifanya mazoezi ya mpira wa kikapu kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kocha Mafunzo akiri bado hawajaimarika*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kufanikiwa kufuta vumbi la kupoteza michezo minne mfululizo, Kocha Mkuu wa Klabu ya Maafande wa Mafunzo, Abdalla Bakari 'Edo', amesema bado timu yake haijaimarika vizuri kuweza kushindana katika mbio hizo za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar.

Juzi katika Uwanja wa Mau A, Mafunzo iliichapa Ngome FC bao 1-0, ushindi huo ukija baada ya kupoteza mechi nne zilizopita kwenye ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Bao hilo pekee la Mafunzo lililodumu kwa dakika zote 90 za mchezo, liliwekwa nyavuni na Abdul Naim katika dakika ya 45.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Kocha Mkuu wa Mafunzo, Edo alisema licha ya kupata alama tatu lakini bado timu yake haijaimarika vizuri.

Alisema mchezo huo umempa njia ya kuendelea na mbinu zake za kubadilisha aina ya uchezaji na mfumo wanaotumia hasa wanapokutana na timu ambazo zinauhitaji ubingwa na zile zinazopigania kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Edo alisema mchezo huu ambao wamepata alama tatu ndio ulikuwa mgumu zaidi kuliko yote kwa kuwa wapinzani wao wana malengo ya kuibakisha timu hiyo Ligi Kuu kama ilivyo kwao.

"Tumecheza na timu ambayo ipo kama sisi katika mwenendo mbaya wa kupata matokeo tangu kuanza msimu, hivyo haukuwa mchezo rahisi kwa kuwa kila mmoja alikuwa akitaka ushindi wa alama tatu," alisema.

Aidha, alisema baada ya kufanikiwa kupata alama tatu katika mzunguko huu wa 10, sasa wanajipanga kwa mchezo wao wa 11 ambao watakutana na timu ya Jamhuri kutokea Kisiwani Pemba kesho, Jumatano utakaopigwa katika Uwanja wa Mau A majira ya saa kumi alasiri.

Mafunzo kwa sasa imefikisha alama 10 ikiwa nafasi ya 11 alama sawa na mpinzani wao Jamhuri waliopo nafasi ya 12.

# Choki aifufua tena bendi ya Extra Bongo

**Na Sabato Kasika**

BAADA ya kuzunguka bendi mbalimbali kwa muda mrefu, hatimaye mwimbaji nyota wa muziki wa dansi, Ally Choki, ameamua kufufua bendi yake ya Extra Bongo.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Choki alisema bendi hiyo itaingia kambini wiki ijayo, ili kujifua kwa nyimbo mpya na za zamani ambazo iliwahi kutamba nazo.

"Kwa sasa ninaendelea kukusanya wanamuziki, kwa ajili ya kambi ya mazoezi kwa muda wa wiki ambazo ninaamini tutatoka tukiwa tumeiva tayari kutoa burudani," alisema Choki.

Choki alifafanua kuwa Extra Bongo ya sasa itakuwa na sura nyingi mpya pamoja na baadhi ya waimbaji wakongwe akiwamo Rogert Hegga 'katapila'.

Alisema hakuwa na mpango wa kufufua bendi hiyo, lakini wadau wa muziki wa dansi wamemshawishi na kuahidi kuwa naye bega kwa bega ndipo akachukua uamuzi huo.

"Tangu awali sikuwa na mpango, lakini wakati mwingine mtu unalazimika kusikiliza ushauri wa watu kama unaona unafaa, ndivyo nilivyofanya," alisema.

Itakuwa ni mara ya tatu Choki kurejesha bendi hiyo ambayo imewahi kumfia mikononi mara mbili alipoianzisha mwanzo mwaka 2004 na kuleta upinzani kwenye muziki wa dansi ikitamba na nyimbo mbalimbali ukiwamo wa '3x3', Mjini Mipango' na nyingine nyingi.

Mwaka 2005 aliungana na Mwinjuma Muumin na kuanzisha Bendi ya Doble Extra ambayo haikudumu sana akaamua kurudi Twanga Pepeta, baadaye akatoka na kufufua Extra Bongo.

Hata hivyo, haikudumu kwa muda mrefu, ikafa mwaka 2014 ambapo tangu muda huo amezunguka katika bendi mbalimbali ikiwamo Super Kamanyola ya Mwanza na Twanga Pepeta. Sasa ameamua kurejesha tena bendi yake ambayo ilikufa karibu miaka 10 iliyopita.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CITY WAMTAKA JAMES

KLABU ya Manchester City inavutiwa na mlinzi wa Chelsea na England, Reece James, 23, kama mbadala wa muda mrefu wa Kyle Walker, 33. ***(Independent, via Manchester Evening News)***

### MADRID YAKOMAA NA DAVIES

KLABU ya Real Madrid bado inamuwania Beki wa Bayern Munich na Canada, Alphonso Davies mwenye umri wa miaka 23. ***(Fabrizio Romano)***

### KELLY LULU SPURS, LIVER

LIVERPOOL na Tottenham zitalazimika kulipa hadi pauni milioni 30 kumnunua mlinzi wa Bournemouth, Lloyd Kelly, 25, wakati wa dirisha la uhamisho la Januari litakapofunguliwa. ***(Football Insider)***

### MILAN YAVUTIWA NA BOTELI

KLABU ya Inter Milan inavutiwa na mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach raia wa Uswisi, Winsley Boteli, 17, ambaye pia ananyatiwa na Everton. ***(Inter Milan Live, Liverpool Echo)***

### GRAY ATUMIWA MASKAUTI

LIVERPOOL wametuma maskauti wao huko Leeds mara kadhaa kumfuatilia kiungo wa England, Archie Gray, 17. ***(Caught offside)***

### WILLIAMS HATAKI KUONDOKA

WINGA wa Hispania, Nico Williams, 21, hataki kuondoka Athletic Bilbao na huenda akakubali kutia saini mkataba mpya na klabu hiyo ya Hispania, jambo ambalo litafanya iwe vigumu kwa Aston Villa kumsajili mchezaji huyo Januari. ***(Birmingham Live)***

### NDIDI ATAKIWA BARCA

BARCELONA ina nia ya kumsajili kiungo wa Nigeria, Wilfred Ndidi, 26, mkataba wake na Leicester City utakapokamilika mwishoni mwa msimu. ***(Sky Sports)***

### GREENWOOD KUBAKIZWA

KLABU ya Getafe inamtaka mshambuliaji wa zamani wa England, Mason Greenwood, 22, abakie nao kwa mkopo kutoka Manchester United. ***(Sun)***

### BARDGHAJI AWANIWA NICE

BILIONEA Sir Jim Ratcliffe, 71, ambaye anamiliki Klabu ya Nice ya Ufaransa na anayetarajiwa kuwa mmiliki mpya wa Manchester United, ana nia ya kumleta kiungo wa kati wa Sweden, Roony Bardghji, 17, kwenye klabu yake hiyo ya Ligue 1 baada ya kutoka kwenye benchi na kufunga bao la ushindi kwa FC Copenhagen dhidi ya United. Chelsea, Newcastle na Crystal Palace pia wanamuwania. ***(Sun)***

### FABREGAS KOCHA COMO

KIUNGO wa kati wa zamani wa Hispania, Chelsea na Arsenal, Cesc Fabregas, 36, anatazamiwa kuteuliwa kuwa kocha mkuu mpya wa Como katika nafasi yake ya kwanza ya ukocha mkuu. ***(Fabrizio Romano)***

### KUSAJILI MSHAMBULIAJI

CHELSEA inatazamia kusajili mshambuliaji Januari licha kiungo wa kimataifa wa Senegal, Nicolas Jackson, 22, kufunga mabao manne katika mechi zake mbili zilizopita za Ligi Kuu England. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# POCHETTINO AMWOMBA RADHI PEP NA WAAMUZI

**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino ameomba msamaha kwa Pep Guardiola na wasimamizi wa mechi baada ya kuonesha hasira yake mwishoni mwa mchezo wa sare ya mabao 4-4 kati ya Chelsea na Manchester City katika mchezo wa Ligi Kuu England uliopigwa Uwanja wa Stamford Bridge juzi, Jumapili.

**Kocha huyo wa Chelsea aliingia uwanjani kubishana na mwamuzi Anthony Taylor baada ya kumalizika mchezo wakati Chelsea walipokuwa wakitafuta bao la tano.**

Pochettino alikataa kupeana mkono na Kocha wa City, Guardiola na alioneshwa kadi kwa kugombana na Taylor, kabla ya kuburutwa na wafanyakazi wawili mwishoni mwa mechi hiyo kali ambayo timu yake ilipata sare kupitia kwa Cole Palmer dakika ya 95 kwa mkwaju wa penalti.

"Nahitaji kuomba msamaha kwa Anthony (Taylor) na maafisa wote," alisema Pochettino.

**●●● Nilistahili kuadhibiwa kwa sababu nilivuka kikomo, si taswira nzuri kwangu na kwa...**

"Katika wakati ule nilihisi Raheem (Sterling) anaweza kufunga bao la tano. Katika wakati ule tulipomaliza mchezo, nilimgeukia Anthony na kusema 'Nini, unajua, kinaendelea? Kwa nini umalize wakati huu.?'

"Kisha, niligeuka na kusema 'nilistahili kuadhibiwa' kwa sababu ndiyo, nilivuka kikomo. Nataka kuomba radhi kwa sababu si taswira nzuri kwangu na kwa soka, aina hii ya tabia."

Akiwa amemsukuma na kumpuuza na kumsukuma Guardiola, Pochettino alisema: "Nataka kumuomba msamaha pia. Katika wakati huu, sikumuona. Nililenga tu kitendo. Kwa hiyo nataka kumuomba msamaha Pep pia."

Guardiola alipoulizwa kuhusu tabia hiyo alijibu, "Hakuna shida."

"Sio shida. Sitaki kuongelea hilo, ni sawa. Kila mtu mwenye hisia, ilinitokea wakati mwingine. Ni sawa, kwa uaminifu. Sitaki unielewe vibaya zamani ilifanyika na Pochettino lakini ni sawa kabisa."

Mkwaju wa penalti wa Erling Haaland dakika ya 25 uliipa City bao la kuongoza kabla ya Thiago Silva na Sterling kufunga bao la wenyeji.

Manuel Akanji aliisawazishia City katika muda wa dakika za mwisho za kipindi cha kwanza na kisha Haaland akafunga na kuwapa wageni uongozi wa mabao 3-2 katika dakika 47.

Nicolas Jackson alisawazisha tena dakika ya 67 kabla ya Rodri kuachia shuti kali dakika ya 86 kuonekana kuipa City pointi zote tatu. Lakini Ruben Dias alimfanyia madhambi Armando Broja kwenye eneo la hatari na Palmer akafunga penalti dhidi ya klabu yake ya zamani.

City wako kileleni mwa Ligi Kuu wakiongoza kwa pointi moja kuelekea mapumziko ya kimataifa ambapo Chelsea wanashika nafasi ya kumi kwa pointi 16.




# MAGUIRE: UVUMILIVU UMEZAA MATUNDA

**MANCHESTER,** England

HARRY Maguire amesema uamuzi wake wa kubakia Manchester United msimu wa majira ya joto umezaa matunda baada ya kurejea katika kikosi cha kwanza cha kocha, Erik ten Hag.

Baada ya msimu wa kwanza kusumbuka chini ya Ten Hag, Maguire alikaribia kuhamia West Ham United wakati wa dirisha la usajili la majira ya joto, lakini akaishia kubakia Old Trafford.

Alianza kampeni ya sasa kwenye benchi, lakini ameanza mechi nane zilizopita katika mashindano yote na anaamini inaonesha alikuwa sahihi kubaki United.

"Nilicheza mechi chache mwaka jana, 16 au 17 nilianza, na nilihisi kama nilifanya vema katika michezo niliyocheza, sikucheza kama ningependa," alisema Maguire.

"Kwa upande mwingine, Rapha (Raphael Varane) na Licha (Lisandro Martinez) walikuwa wakicheza kwa ustadi na walitengeneza upatina mzuri.

"Nililazimika kutumia muda wangu na kuwa mvumilivu. Nilipata nafasi mbili au tatu msimu uliopita wa kukimbia lakini niliugua, niliugua majeraha mara mbili, kwa hiyo sikupata mdundo wangu, lakini sasa michezo ambayo nimeweza kucheza inajidhihirisha kwa kocha juu ya kiwango changu.

"Ninafurahia sana soka langu na ninafurahia sana kuichezea klabu hii. Nilikuwa tayari kubaki na kupigania nafasi yangu na tuna mabeki wa kati wanne au watano wa juu katika klabu hii na ushindani wa nafasi ni mkubwa sana."



# Xavi alia na vyombo vya habari

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez, amesema shutuma za vyombo vya habari zimeathiri uchezaji bora wa wachezaji wake vijana, baada ya timu yake kutoka nyumba na kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Alaves Jumapili kwenye Uwanja wa Olympic.

Barca walikuwa wamepoteza mechi mbili kati ya tatu zilizopita kabla ya ziara ya Alaves na walizomewa hadi mapumziko baada ya Samu Omorodion kuwapa wageni bao la kuongoza la kushtukiza baada ya sekunde 17 pekee.

Robert Lewandowski alifunga mabao mawili katika kipindi cha pili na kuifanya Barca kusalia na pointi nne dhidi ya vinara wa LaLiga Girona, lakini ushindi huo haukupunguza shinikizo kwa timu ya Xavi ambayo haikufanya vizuri.

"Tulianza kwa mguu wa nyuma," alisema Xavi katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mchezo.

"(Ilkay) Gundogan alipoteza mpira ambao hangepoteza kwa kawaida na kuna mabadiliko. Hatuwezi kuruhusu makosa haya, haikubaliki.

"Tunazipa timu vitu vingi sana. Tumepoteza pointi huko Mallorca, Granada... Tunatoa nyingi sana na inaleta hali ya kutojiamini miongoni mwa wachezaji ambayo si nzuri.

"Wakati wa mapumziko, niliwaambia watulie na tukicheza soka letu tutarudi, wachezaji walikuwa na wasiwasi kuliko kawaida kwa sababu ya kila kitu kinachozalishwa karibu na timu, na sio haki.

"Sio haki kwa sababu kumekuwa na majeruhi na wachezaji kurejea. Tunapaswa kujikosoa pia, lakini ni kawaida kwamba hatuwaoni wachezaji wakiwa katika ubora wao kwa sababu hawajisikii kuwa huru."

Baada ya kushindwa na Real Madrid, ushindi mwembamba dhidi ya Real Sociedad na kupoteza kwa Shakhtar Donestsk katikati ya wiki, Barca imeshutumiwa vikali na vyombo vya habari na Xavi alisema hilo limewasumbua wachezaji wachanga zaidi.

"Bila shaka kile ambacho vyombo vya habari vinasema huathiri jinsi timu inavyocheza," aliongeza.

"Vyombo vya habari vinaunda hali ambazo kwangu si za kweli. Na inaathiri, timu bila shaka yoyote.

# Klopp amsifu Nunez kwa kiwango bora

**LIVERPOO,** England

KOCHA Jurgen Klopp ametoa sifa maalum kwa Darwin Nunez baada ya Liverpool kushinda mabao 3-0 dhidi ya Brentford, Jumapili.

Fowadi huyo amekuwa akilaumiwa wiki iliyopita kwa kushindwa kuleta matokeo katika mchezo wowote wa 'Wekundu' hao dhidi ya Luton Town na Toulouse - hata kukosa bao la wazi katika mechi iliyofanyika Kenilworth Road.

Uchezaji wake ulimfanya mchezaji wa zamani wa Liverpool, Jose Enrique kusisitiza kwamba fowadi huyo 'hatakuwa mshambuliaji wa kiwango cha kimataifa'.

Wakati Nunez kwa mara nyingine alishindwa kufunga bao katika ushindi dhidi ya Brentford - kuona mpira wa juu ukikataliwa – uchezaji wa raia huyo wa Uruguay ulikuwa mzuri sana.

Mshambuliaji huyo alifunga bao la kwanza la ushindi na kuifanya Liverpool kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Anfield.

Akizungumza baada ya mchezo kumalizika kwa waandishi wa habari, Klopp alipenda kusifu namba yake tisa, huku akimsifu Nunez kwa uchezaji wa kustaajabisha na kiwango chake cha ulinzi.

"Jinsi tulivyodhibiti nyakati ambazo tunaweza kudhibiti ilikuwa ya kipekee kabisa. Nyakati zote tulipoweza kuweka mpira chini, tulipoweza kucheza kandanda, Darwin alipounganisha mchezo kwa kipekee, tulikuwa hatari sana kwa wapizani wetu.

"Tunaweza kushawishi kuwa na mchezaji mmoja, unapoanza kushinikiza kutoka katikati lazima uende kwa goli, bila kupata mpira, anapiga pasi hadi katikati na unafuata. Kiwango cha kazi kilikuwa cha kichaa."



HABARI MICHEZO

# MABAO 159 YAFUNGWA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya mabao 159 yamefungwa hadi kufikia raundi ya tisa ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambapo kwa sasa imesimama kupisha mechi za Kalenda ya FIFA, huku baadhi ya wachezaji wakiwa wamekwenda kuzitumikia timu zao za taifa.

Idadi hiyo ya mabao imefungwa na jumla ya wachezaji 99, kwa mechi 71 ambazo zimechezwa mpaka sasa.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu cha Dawati la Michezo la Nipashe, kati ya mechi hizo, michezo 50 imetoa mshindi, na 21 timu zikitoka sare.

**Takwimu zinaonyesha kuwa kati ya mechi 50 ambazo zimetoa washindi, idadi ya mechi 30 timu zimeshinda nyumbani na michezo 20 timu zikishinda ugenini.**

Jumla ya penalti 11 zimetolewa mpaka sasa na tisa zikiwekwa wavuni, mbili zikiota mbawa.

Yanga inayoongoza kufunga mabao 26 mpaka sasa, 16 yamefungwa kwa mguu wa kulia, saba mguu wa kushoto na matatu kwa vichwa.

Jean Baleke wa Simba ambaye ana mabao saba kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, yote amepachika kwa mguu wa kulia huku, Stephane Aziz Ki ambaye naye ameshacheka na nyavu mara saba, amepachika mabao manne kwa mguu wa kushoto na kumfanya kuwa kinara kwa kufunga mengi zaidi mpaka sasa na matatu mguu wa kulia.

Straika wa Singida Fountain Gate, Habib Kyombo, anaongoza kwa kupachika mabao kwa vichwa akiwa amefanya hivyo mara tatu, ikiwa pia ni idadi ya mabao ambayo ameyafunga mpaka sasa.

Maxi Nzengeli wa Yanga ndiye mchezaji pekee mwenye mabao saba, moja likiwa la kichwa. Mabao, manne ameyafunga kwa mguu wa kulia, mawili mguu wa kushoto, na kutimiza idadi ya mabao saba ambayo amefunga kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.




## KMC yampa tano kocha wake kuifanya kuwa tishio

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imempa pongezi kubwa kocha wake, Abdihamid Moalin, kwa kuifanya timu hiyo iwe ya ushindani na tishio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

Akizungumza kwa niaba ya uongozi wa klabu hiyo, Kaimu Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Khalid Chukuchuku, alisema wanampa pongezi kubwa kwa kuibadilisha KMC, ambapo si ile ya msimu uliopita, badala yake ameifanya kuwa timu na si kikundi cha wachezaji.

"Moalin ameifanya timu imekuwa na ushindani mkubwa ukilishanganisha KMC ya msimu huu na iliyopita kuna vitu vingi unaviona kabisa vipo tofauti.

Timu yetu ina wachezaji 32 walio kwenye kikosi cha msimu huu, na wote wamepata nafasi ya kucheza, hakuna mchezaji abiria ambaye yeye amekaa tu anaangalia wenzake, hiyo ina maana kocha anamwamini kila mchezaji aliyenaye kwenye kikosi na kila anayepewa nafasi anaonyesha kile ambacho anacho, lakini kikubwa ni vile anavyokiunganisha kikosi, kambini na kwenye mazoezi ameifanya kuwa timu, tena timu ya kutisha, kuna zingine ni vikundi tu vya wachezaji," alisema Kaimu Ofisa Habari huyo.

Alisema ukiangalia KMC kwenye msimamo wa Ligi Kuu kwa sasa inaonyesha kuwa si timu ya masihara msimu huu na itakuja kushangaza watu mbele ya safari.

"Tumecheza michezo tisa ya Ligi Kuu, tuko nafasi ya tano pointi 15 sawa na Dodoma Jiji ambao wako nafasi ya nne, lakini ni tofauti ya pointi nne na timu iliyo nafasi ya pili na ya tatu kwa hiyo unaona msimu huu tuko vizuri, naona timu yetu msimu huu inakwenda mbali, na usishangae tukarudi kucheza mechi za kimataifa kama miaka kadhaa iliyopita.

VIPAJI...




Vijana wa Kituo cha kukuza vipaji cha Jakaya Kikwete wakiwania mpira wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya kituo hicho jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Simba yaanika siku kocha mpya kutua*

INATOKA UKURASA 24

pamoja na kwamba tumecheza mechi chache ambazo ni mbili, lakini ya hapa nyumbani dhidi ya Al Ahly Oktoba 20, tulionesha ni jinsi gani tupo bora na ikasababisha waandaaji wa michuano ya African Football League, Shirikisho la Soka Afrika (CAF), na FIFA kutupa tuzo," alisema.

Alisema tuzo hiyo imewafanya kuwa na kiu ya kutengeneza kikosi bora zaidi kitakachoakisi ubora wa mashabiki.

"Hii imetuheshimisha sana na imefungua ukurasa mpya wa mashabiki wa Simba duniani, ambacho kinatakiwa sasa ni ubora wa mashabiki nje ya uwanja, sasa uelekezwe pale uwanjani kwenye 'pitch', ili vitu viwili viende kwa pamoja," alisema.

## Gamondi aivalia njuga Belouizdad

INATOKA UKURASA 24

Gamondi alisema anaendelea kuangalia baadhi ya mechi na kuwafuatilia CR Belouizdad jinsi wanavyocheza michezo ya nyumbani na kuona ubora wao.

Yanga imetinga makundi ikiwa ni miaka 25 tangu ilipofika hatua hiyo kwa mara ya kwanza mwaka 1998, ikiwa ni miezi michache baada ya kucheza fainali ya Kombe la Shirikisho na kupoteza kwa faida ya bao la ugenini dhidi ya USM Alger.

# Michezo

Jumanne Novemba 14, 2023

Nipashe





## Klopp amsifu Nunez kwa kiwango

UKURASA 22



Kocha wa zamani wa USM Alger, Abdelhak Benchikha na aliyekuwa kocha wa viungo wa Simba, Adel Zrane (picha ndogo chini), ndio wanaopewa nafasi kubwa ya kurithi mikoba ya Robertinho Oliveira na Corneille Hategekimana katika klabu hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAANIKA SIKU KOCHA MPYA KUTUA

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

## ●●● Yaiendea 'msituni' Asec Mimosas huku ikieleza Tuzo ya Mashabiki AFL itaongeza...

WAKATI uongozi wa Simba ukiendelea na mchakato wa kuziba nafasi ya benchi la ufundi, Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Daniel Cadena, amesema wameanza maandalizi ya kukisuka kikosi chao kuelekea mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Asec Mimosas ya Ivory Coast.

**Simba imeingia kambini jana kwa wachezaji ambao hawako kwenye majukumu ya timu za taifa kuendelea na maandalizi ya mchezo wa kwanza wa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa utakaochezwa Novemba 25, mwaka huu, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Cadena anashirikiana na Seleman Matola kukiimarisha kikosi cha timu hiyo huku wakiendelea kuwafuatilia wapinzani wao Asec Mimosas lengo likiwa wanapata matokeo mazuri katika mchezo wao huo wa kwanza wa hatua ya makundi.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Cadena alisema baada ya kutopata matokeo mazuri katika michezo miwili iliyopita ya Ligi Kuu Bara, wameona madhaifu yao na kuanza kuyafanyia kazi.

"Kazi kubwa ni kuendelea kuimarisha safu ya ulinzi kutoruhusu mabao na ushambuliaji kuwa makini na utulivu kwenye nafasi wanazotengeneza ili kupata mabao.




Mechi iliyopita dhidi ya Namungo FC, tulitengeneza nafasi na kushindwa kuzitumia na sasa tunaanzia hapo kufanyia kazi kwa washambuliaji wetu na kuwasisiza mabeki kuwa na utulivu ili kutorudia makosa hayo," alisema Cadena.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema mchakato wa kutafuta Kocha Mkuu unaendelea, wiki hii watamtambulisha rasmi mrithi wa Robertinho Oliveira.

Aliongeza kuwa wametafuta kocha aliyekuwa bora na mwenye uzoefu mkubwa na soka la Afrika ili kuweza kuisaidia Simba kufikia malengo yake katika mashindano ya ndani na kimataifa.

Akizungumzia tuzo ya mashabiki waliyozawadiwa katika michuano ya African Football League (AFL), iliyomalizika juzi nchini Afrika Kusini na Mamelodi Sundowns kuwa mabingwa kwa kuifunga Wydad Casablanca ya Morocco mabao 2-0, ikiwa na ushindi wa jumla wa mabao 3-2 baada ya kupoteza 2-1 ugenini kwenye fainali ya kwanza, Ahmed alisema ni jambo la kujivunia na itakuwa imeleta faraja na subira kwa mashabiki wao.

"Sisi kama Simba tumefurahi kupata tuzo hii, ni tuzo ambayo inaashiria uhalisia kwa asilimia 100, mashabiki wa Simba walistahili kwa sababu ya ubora waliokuwa nao wa kushangilia na kuleta hamasa uwanjani, ukitazama mashindano haya,

INAENDELEA UKURASA 23

# Gamondi aivalia njuga Belouizdad

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema baada ya kufanya vizuri katika michezo tisa ya Ligi Kuu Bara, nguvu na akili zao wanazihamishia kimataifa kwani anataka kuweka rekodi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga inatarajiwa kusafiri kuelekea nchini Algeria kwa ajili ya mchezo wao wa kwanza wa hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CR Belouizdad ambayo Gamondi amewahi kuinoa miaka ya nyuma.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema anaimani na ubora wa kikosi chake kwa kufanya vizuri katika mchezo wao wa ugenini dhidi ya wapinzani wao hao kuwa kwenye kiwango bora.

Alisema uwajibikaji wa wachezaji wake uwanjani ni sehemu ambayo inampa matumaini ya kufanya vizuri katika mchezo wa kimataifa na kuhakikisha wanaweka rekodi.



"Kitendo cha kufanya vizuri katika mechi za ndani na tulipofanikiwa sasa tunapata mwanga mzuri kuelekea michuano ya kimataifa, akili yetu sasa imehamia kimataifa kujiandaa dhidi ya CR Belouizdad.

"Tunahitaji kuweka rekodi kwa kuvuka hatua hii na kusonga mbele zaidi kwa kucheza robo fainali ya michuano hii mikubwa," alisema Gamondi.

Aliongeza kuwa hawahitaji kuishia katika hatua ya makundi kwani malengo yao makubwa ni kuona wanafanikiwa kuvuna alama tisa za nyumbani na kutafuta pointi muhimu ugenini ili kutinga robo fainali.

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >